# Nipashe

Jumamosi Machi 14, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580179

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Mmiliki wa mabasi ya J4 Express ahukumiwa kunyongwa hadi kufa

UKURASA 3




UKURASA 13

# Magufuli sasa avalia njuga virusi Corona

**ATAKA** tahadhari, elimu itolewe kila kona, nchi jirani Kenya, Congo zatikiswa...*Endelea ukurasa wa 2*




Rais John Magufuli, akiwa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo na Balozi wa Ujerumani nchini, Regine Hess, wakifunua pazia kuashiria uzinduzi wa karakana kuu ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Lugalo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**



## BAA LA CORONA

KENYA na Ethiopia zimethibitisha kuwa na wagonjwa wa Corona huku Waziri Mkuu wa Canada, Justin Trudeau, akilazimika kuwekwa karantini kwa siku 14 baada ya mkewe, Sophie Gregoire, kukutwa na virusi hivyo. Chukua tahadhari.

## VIGOGO UPINZANI AFRIKA KUTIA JOTO MKUTANO ACT WAZALENDO

UKURASA 3

# Vigogo Chadema mbaroni Mbowe akitoka gerezani

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** YANGA WAMZINGUA EYMAEL, AITAJA SIMBA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Magufuli avalia njuga Corona

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amesema licha ya Tanzania kutokuwa na mgonjwa wa Corona aliyeripotiwa, kuna haja makundi yote kwenye jamii kuchukua tahadhari kuhusu mlipuko wa virusi hivyo.

Vilevile, amesema tayari ameshatoa maagizo kwa Katibu Mkuu Kiongozi kuwa hawatatoa vibali vya watu kusafiri safari wanavyotaka bila sababu za msingi.

Rais Magufuli alitoa tahadhari hiyo jana jijini Dar es Salaam alipozindua karakana kuu la kisasa iliyojengwa na Serikali ya Ujerumani kwa gharama ya Sh. bilioni 8.5 katika Kikosi cha 501 cha Lugalo cha Jeshi la Wananchi (JWTZ).

Alisema mpaka jana wakati anazungumza, Tanzania ilikuwa haijapata mgonjwa wa Corona na kuvitaka vyombo vya ulinzi na usalama visimamie mipaka ili kila anayeingia achunguzwe.

Kiongozi huyo wa nchi alisema kwa sasa ugonjwa huo upo duniani na umekumba nchi nyingi na takwimu zinaonyesha zaidi ya watu 112,000 wameambukizwa na watu 4,500 wamepoteza maisha.

"Ni ugonjwa mbaya, kwa sababu ugonjwa huu umesambaa kila mahali, Tanzania bado hatujapata mgonjwa, lakini hatuwezi kujiweka pembeni bila kuchukua hatua, zimeanza kuchukuliwa, Waziri wa Afya (Ummy Mwalimu) amezungumza na kutoa tahadhari.

"Ni vizuri tuchukue tahadhari kwa nguvu zote, ugonjwa huu unaua na unaua kwa haraka sana, Watanzania tusiupuuze hata kidogo," alitahadharisha.

Alisema ni lazima wananchi waanze kuchukua hatua za kujikinga na tatizo hilo na kuwataka wale wanaopenda kusafiri, kama safari siyo ya lazima, wasifanye hivyo.

"Hata Watanzania wenyewe, wenye mazoea ya kusafiri mkoa huu mara kule, unakwenda kukutana na watu huwajui, mpunguze safari zenu mjilinde na tatizo hili.

"Tatizo hili lipo na tusipuuze, zile tahadhari tunazopewa tusipuuze, tusishikane mikono, tusibusiane, sifahamu usiku watafanyaje, huwezi kukwepa usibusu, mambo yatawezekana tu na ni raha tu, ni vyema tuchukue tahadhari," alisema.

Rais Magufuli pia aliwataka Watanzania wasiwaachie viongozi peke yao kuzungumzia suala hilo.

"Kila mmoja kwenye familia atoe tahadhari, kwenye shule, walimu watoe tahadhari kwa wanafunzi, vyuo, kwenye majeshi, kambini kwenye magari, ikiwezekana kabla ya kupanda kwenye daladala, kondakta atoe tahadhari ili tudhibiti tatizo hili.

"Ugonjwa huu unaharibu uchumi, hata katika maandiko ya zamani zipo tahadhari zilikuwa zikitolewa, wakati wa Nuhu zilitolewa watu wakadharau, Sodoma na Gomola zilitolewa watu wakadharau, Watanzania tahadhari hizi zinazotolewa tuzizingatie.

"Waandishi wa habari ikiwezekana kila siku mhariri atoe tahadhari, angalau hata maneno mawili au matatu, kwenye televisheni au redio kabla ya kutangaza taarifa ya habari, pawapo na mistari miwili ya kupambana na Corona.

"Tukidharau ndugu zangu tutakwisha, mpaka leo dawa hazijapatikana wanatibu dalili. Ninawaomba sana Watanzania, kupitia ujumbe huu, ikawaguse.

"Nchi nyingi zimetoa tahadhari, nchi nyingi zenye mashirika ya ndege zimeacha kutoa huduma ya safari kwenda nchi tofauti, zimepunguza safari, hata sisi ndege inayokwenda India jana (juzi) ikirudi leo (jana) haitakwenda," alisema.

Rais Magufuli pia aliwaomba viongozi wa dini waendelee kumwomba Mungu aiepushe nchi na ugonjwa huo.

"Mungu anaweza kila kitu, kila mmoja katika imani yake, tukamwombe Mungu atusaidie ili janga hili pamoja na tahadhari tunazozichukua hili lisifike Tanzania, tunaendelea vizuri kiuchumi lakini janga hili litaturudisha nyuma likiingia, tuepuke mikusanyiko isiyo ya lazima," alisisitiza.

Rais Magufuli alisema Shirika la Afya Duniani (WHO) limetangaza kuwa Corona ni janga la kidunia, hivyo lazima Tanzania ichukue tahadhari ambayo ni muhimu zaidi kuliko kutibu.

"Vyombo vya habari mkilisimamia hili tutashinda vita hii, unapopiga muziki weka na tangazo la Corona ili wakati mtu anacheza na kubinuka amevaa ... (alitaja nguo ndani), atavaa gauni kwa kusikia neno Corona.

"Wekeni hata dakika moja ya kuelimisha Corona, viongozi wote wa mikoa na tarafa ni jukumu lenu kuelimisha, tuchukua tahadhari kuanzia leo (jana)," aliagiza.

Kuhusu karakana hilo ya jeshi, Rais Magufuli alisema itatumika kutengeneza magari ya kijeshi na kutoa mafunzo ya ufundi siyo kwa jeshi pekee, bali kwa wananchi kwa ujumla.

Rais Magufuli alitoa wito kwa jeshi hilo kulitumia vizuri na kuvitunza vifaa vilivyokabidhiwa na vingine vitakavyoletwa.

"Karakana hii iwe chachu ya kuwaimarisha kiufundi na kuchochea maendeleo ya nchi, ugunduzi mwingi wa masuala ya sayansi na teknolojia umefanyika kwenye majeshi, nawashukuru sana Ujerumani kwa msaada huu.

"Hii ndiyo ndoto yangu, natamani siku moja kuona jeshi linatengeneza silaha na vifaa vyake yenyewe, ninatamani kuona siku moja Watanzania wananunua vifaa au magari yanayotengenezwa na Jeshi la Tanzania," alisema.

Alibainisha kuwa Jeshi la Tanzania ni miongoni mwa majeshi imara na bora duniani na limetoa mchango mkubwa katika harakati za ukombozi na ulinzi barani Afrika, hivyo likiamua linaweza.

"Mbali ya ufadhili huu, Ujerumani imekuwa ikitoa misaada mbalimbali, imejenga vyuo vya kijeshi kwa gharama ya Sh. bilioni 5.6, wametoa vifaa vya askari wanaolinda amani.

"Balozi wao ameeleza hapa, msaada huu mkubwa utatoa mchango mkubwa kwa wanajeshi na raia, mmeienzi ndoto ya Mwalimu Julius Nyerere, aliamua mwaka 1973, Dodoma iwe makao makuu ya nchi, mmejenga Hospitali ya Kijeshi Dodoma, tunashukuru sana," alisifu.

Rais Magufuli alisema mpaka sasa Tanzania imenufaika na misaada kutoka Ujerumani yenye thamani ya Euro bilioni 2.5 na wamekuwa washirika wakubwa wa kiuchumi kwenye nyanja za kibiashara, uwekezaji na utalii.

# Vigogo Chadema mbaroni Mbowe akitoka gerezani



Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika (katikati), Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche (kushoto) na Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salumu Mwalimu (wa pili kulia), wakiwasili katika Makao Makuu ya chama hicho, Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kulipiwa faini na kuachiwa huru kutoka Gereza la Segerea. PICHA: MIRAJI MSALA

**Na Mary Geofrey**

WAKATI Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, akilipiwa faini na kutoka gerezani, baadhi ya vigogo wa chama hicho walikamatwa na vyombo vya dola walipokuwa wakienda kumpokea kiongozi huyo kwenye Gereza la Segerea.

Waliokamatwa ni pamoja na Mwenyekiti wa Wanawake wa Chadema na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, Meya wa Ubungo, Boniface Jacob, na kada wa hicho, Kilewo Mwanga, huku wafuasi wengine wa chama hicho wakitawanywa kwa mabomu.

Tukio hilo lilitokea jana saa 7:30 mchana wakati wafuasi hao, walipokuwa wanakwenda kwenye gereza hilo baada ya kukamilisha malipo ya faini ya Sh. milioni 70 aliyotakiwa kulipa Mbowe baada ya kuhukumiwa Jumanne na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini.

Askari Magereza walitumia silaha za moto na kufyatua risasi hewani kuwatawanya wafuasi wa chama hicho waliokuwa nje ya gereza hilo kumsubiri Mbowe.

Katika tukio hilo, baadhi ya viongozi na wananchi kadhaa walijeruhiwa, akiwamo dereva wa bodaboda aliyedaiwa kuvunjika mguu.

Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, alithibitisha kutolewa kwa Mbowe gerezani na kukamatwa kwa makada hao na kusema kuwa suala hilo wanalifuatilia wakati wakimsubiri mwenyekiti wao kuwasili makao makuu Kinondoni jijini.

Nipashe ilizungumza na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Ilala, Zuberi Chembela, ambaye alikiri kukamatwa kwa watu 27 ambao ni wafuasi wa Chadema kwa tuhuma za kufanya vurugu eneo la magereza.

Alisema watuhumiwa wote wako Kituo cha Polisi Stakishari jijini kwa ajili ya mahojiano na akasisitiza kuwa dhamana zao zilikuwa wazi baada ya kukamilisha mahojiano.

HECHE AANIKA MADHILA

Mbunge wa Tarime, John Heche, aliyekuwa miongoni mwa washtakiwa tisa wa kesi ya uchochezi iliyowapeleka gerezani, baada ya kutoka gerezani, alisema namba yake ya ufungwa ni 302, akilalamika kuwa wakati wote kesi yao mahakamani, walinyimwa haki, hivyo alikuwa ameshajiandaa kufungwa gerezani na siyo kulipa faini.

Alisema kwa kipindi cha miaka miwili, kesi dhidi yao iliendeshwa kukiwa na kesi ndogo nyingi ndani yake, hivyo kuliwafanya kujiandaa kufungwa gerezani.

"Mimi nilijiandaa kufungwa na siyo kupigwa faini, nataka tu niseme nilikuwa sawasawa, na nataka niseme sitapigia mtu magoti kwa kitisho cha gereza au cha kuniua, kwa sababu yale ninayoyapigania ninayoamini na nitayasimamia mpaka tone langu la mwisho la damu. Hilo nataka niliweke sawasawa ili kila mtu na kila Mtanzania ajue," alisema.

Heche alisema kwa siku walizokaa magereza walikuwa chuoni kwa sababu wameona mambo mengi ya aibu na ya ajabu.

Alisema mambo yanayofanyika gerezani ni ya kuwadhalilisha Watanzania na yamempa nguvu ya kuendeleza mapambano ya kuiondoa serikali madarakani.

Alidai kuwa wakiwa gerezani, walivuliwa nguo zote, wafungwa wote bila kujali umri wao na kutakiwa kukaa kwenye ndoo ya bati kwa ili kujisaidia haja kubwa.

Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, ambaye pia ni miongoni mwa tisa waliohukumiwa katika kesi hiyo, alisema wakiwa gerezani, walipangishwa foleni wakiwa utupu na kutakiwa kutoa haja kubwa hata kama hauna haja hiyo.

Alisema wamefikia hatua hiyo kwa sababu wamekuwa wakidai haki na demokrasia ya kweli katika nchi yao na mapambano hayo bado yataendelea bila kukatishwa tamaa jambo lolote.

Aliwataka Watanzania kujadili masuala ya msingi badala ya kubadili ajenda na kuanza kufikiria undugu wake na Rais John Magufuli ambao hata chama chake cha Chadema wanautambua.

Alisema Msemaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, si wasemaji wa familia, hivyo hawakuwa na sababu ya kuzungumzia masuala ya familia yake.

Naibu Katibu Mkuu wa Chadema, Salum Mwalimu, ambaye ni sehemu ya waliohukumiwa kifungo cha miezi mitano jela au kulipa faini ya mamilioni ya shilingi, alisema magerezani kuna hali mbaya na hivyo aliwataka Watanzania kuwachangia wafungwa wakristo ambao wanafunga wakati huu wa msimu wa Kwaresma kwa sababu hawana chakula.

Alisema pia kuna matatizo katika ratiba za mahabusi kwenda mahakamani kutoka magerezani kutofautiana hivyo kuwafanya mahabusi kushindwa kufikishwa mahakamani kwa siku zilizopangwa.

Mnyika ambaye pia alihukumiwa pamoja na vigogo hao wa Chadema, alisema hukumu dhidi yao ni sehemu ya mbinu za kuidhibiti Chadema kuiondoa CCM madarakani.

Jumanne iliyopita, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, iliwahukumu vigogo wanane wa Chadema na mwanachama mpya wa CCM, Dk. Vincent Mashinji kulipa faini ya jumla ya Sh. milioni 350 au kwenda jela kutumikia kifungo cha miezi mitano kila mmoja.

Tangu kutolewa kwa hukumu hiyo, wafuasi wa Chadema wamekuwa wakichangishana fedha zilizowezesha kutolewa kwa dhamana vigogo wote waliohukumiwa huku CCM nao wakimlipia faini Dk. Mashinji.

## HABARI KITAIFA

# Mmiliki wa mabasi ya J4 Express ahukumiwa kunyongwa hadi kufa

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

MAHAKAMA Kuu ya Mwanza imemhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa mfanyabiashara na mmiliki wa kampuni ya Mabasi ya J4 Express, Jumanne Mahende, mkazi wa Nyakato wilayani Nyamagana.

Mfanyabiashara huyo, maarufu kama J4, amehukumiwa adhabu hiyo baada ya kutiwa hatiani na kosa la mauaji ya kukusudia kwa kuwapiga risasi watu wawili mwaka 2015. Watu hao ni wafanyabiashara wenzake Ally Abeid na Cloud Sekarwanda

Hukumu hiyo iliyokuwa na kurasa 12, ilitolewa jana na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Mwanza, Sam Rumanyika.

Mahende ambaye ni Mkurugenzi wa kampuni ya Mabasi ya J4 Express, alishtakiwa kwa madai ya kuwapiga kwa risasi Abeid mkazi wa Igoma na Sikarwanda, mkazi wa Nyasaka Ilemela, Julai 13, 2015, majira ya saa 4:00 usiku eneo la Nyakato Boma kwenye ofisi na karakana ya magari yake.

Akitoa hukumu ya kesi hiyo, Jaji Rumanyika alisema mahakama hiyo imejiridhisha kuwa Jamhuri imethibitisha mashtaka dhidi yake bila kuacha chembe ya shaka kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani hapo na mashahidi 12.

Kabla ya kumtia hatiani, Jaji Rumanyika alisema Mahende alitumia nguvu kubwa ya kuvuka mipaka wakati wa kujihami na kwamba nia ya kuua wakati mwingine huwa si dhahiri, hivyo mahakama huangalia aina ya silaha iliyotumika.

Pia alisema mahamaka huangalia sehemu iliyoshambuliwa, matendo ya mshtakiwa kabla na baada ya kufanya mauaji na alifanya mashambulio mangapi kwenye mwili wa marehemu.

Jaji Rumanyika alisema mahakama hiyo haina shaka kuwa bastola iliyotumika kutekeleza mauaji hayo ilikuwa kubwa na kwamba mshtakiwa aliwashambulia vifuani watu hao.

Kwa mujibu wa maelezo ya hukumu hiyo, ushahidi wa Mahende au J4 ( shahidi pekee wa utetezi) ulikinzana na ushahidi wa shahidi wa tano wa Jamhuri kuwa si kweli aliwapiga mgongoni kwa risasi mmoja wa marehemu hao.

Hukumu hiyo ilieleza kuwa mshtakiwa alikiri kuwapo walinzi kwenye eneo hilo (yadi ya magari) wakati anavamiwa alipaswa kupiga kelele kuomba msaada lakini hilo halikufanyika na muda wote alibaki kimya na ukimya huo uliendelea kabla na baada ya tukio hilo, jambo linaloacha maswali bila majibu.

Jaji Rumanyika kwenye hukumu hiyo, alisema ilitegemewa mshtakiwa alipaswa kuwakaribisha watu hao ofisini wakae badala ya kwenye kona ambako alikuwa na mtu mwingine lakini hilo hakulifanya.

Kadhalika, Jaji alisema haishangazi mahakama kuwa mshtakiwa hakuwahi kujisalimisha polisi hadi alipopigiwa simu na alichukua mbinu na tahadhari ya kukwepa mauaji hayo na baada ya mauaji alionyesha kwa vitendo hakujutia mauaji.

Kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani na Jamhuri bila kuacha shaka kwa kuthibitisha mashitaka yao, Jaji Rumanyika alisema mahakama inamhukumu mshtakiwa huyo adhabu ya kifo baada ya kumtia hatiani kwa kosa la mauaji ya kukusudia.

Kwenye shauri hilo la mauji namba 131/2017, upande wa Jamhuri iliwakilishwa na Wakili Robert Kindado akisaidiwa na Mwajuma Feregete na ulitela mashahidi 12 na vielelezo sita huku utetezi ukiwakilishwa na wakili Anthony Nasimire na shahidi mmoja ambaye alikuwa mshtakiwa.

Katika kesi hiyo, ilidaiwa kuwa Julai 13, 2015 Mahende aliwaua kwa kuwapiga risasi wafanyabiashara wanzake wawili, Abeid na Sekarwanda katika eneo la Nyakato Boma lililoko sehemu ya kuhifadhia magari ya kampuni ya mabasi yanayofanya safari kutoka Mwanza kwenda Sirari, mali ya mshtakiwa huyo.



Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP), Simon Sirro, akizungumza na Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC), Dk. Stergomena Tax, aliyemtembelea ofisini kwake Makao Makuu Ndogo ya Jeshi hilo jijini Dar es Salaam jana na kujadiliana masuala mbalimbali ya kiutendaji. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Vigogo upinzani Afrika kunguruma ACT-Wazalendo

**Na MwandishiWetu**

VIONGOZI mashuhuri wa upinzani barani Afrika wanatarajiwa kuzungumza katika mkutano mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo unaoanza leo kwenye Ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa ratiba ya mkutano huo wa siku tatu, mgeni rasmi atakuwa mmoja wa vigogo wa upinzani Zimbabwe, Tendai Biti, anayetarajiwa kutoa hotuba wakati wa ufunguzi wa mkutano huo.

Katibu Mwenezi wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema jana kuwa viongozi wengine mashuhuri wa upinzani wanaotarajiwa kuzungumza katika mkutano huo, ni Jenerali Gregory Muntunyera, maarufu Mugisha Muntu na Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine, wote kutoka Uganda na Mmusi Maimane wa Afrika Kusini.

" Biti anatarajiwa kuwasili nchini leo (jana) usiku na atazungumza baada ya Kiongozi wa Chama, Zitto Kabwe, kufungua rasmi mkutano huo.

" Bobi Wine, Maimane na Muntu hawatakuja nchini kwa sababu ya kubanwa na ratiba zao nyingine za kazi, lakini watatuma ujumbe uliorekodiwa kwa njia ya video na wanachama watawaona moja kwa moja wakiwa ukumbini," alisema.

Mbali na vyama hivyo vya upinzani barani Afrika, mkutano huo unatarajiwa kuhudhuriwa na wawakilishi wengine wa vyama mbalimbali vya Afrika na nje ya Afrika vikiwamo Podemos cha Hispania na Die Linke cha Ujerumani.

Shaibu alisema vyama hivyo vina mrengo wa kijamaa kama ilivyo kwa ACT-Wazalendo.

Huo ni mkutano mkuu wa kwanza wa uchaguzi wa chama hicho tangu kujiunga kwa waliokuwa viongozi wa wanachama wa Chama cha Wananchi (CUF) mwaka jana.

Pamoja na mambo mengine, mkutano huo utafanya uchaguzi wa viongozi wa ngazi za juu wa chama hicho kwa nafasi za Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wa Bara na Visiwani na Kiongozi wa Chama.

Wiki iliyopita, Halmashauri Kuu ya chama hicho iliwapitisha wagombea wanaowania nafasi hizo na kwa mujibu wa Shaibu, watakaowania nafasi hizo ni Nyagaki Shilungushela, Maalim Seif Shariff Hamad na Yeremia Maganja (Mwenyekiti).

Wanaogombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti (Bara) ni Edgar Mkosamali, Dorothy Semu, Shaaban Mambo, Juma Nkumbi, Mary Mongi, Twaha Taslima na Riziki Mngwali. Mwanasiasa mashuhuri wa Zanzibar, Juma Duni Haji atakuwa mgombea pekee wa nafasi ya Makamu Mwenyekiti Zanzibar.

Nafasi ya Kiongozi wa Chama itawaniwa na Zitto Kabwe na Ismail Jussa Ladhu.

Wanachama wa ACT-Wazalendo wanatarajia mchuano mkali zaidi katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti ambayo wamejitokeza wagombea saba.

Kwa mujibu wa tovuti rasmi ya ACT-Wazalendo, mkutano huo unatarajiwa kuhudhuriwa na wajumbe takribani 500 kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani.

# Mkataba uliomvua Lugola wavunjwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MKATABA tata uliosababisha kutumbuliwa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola na Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye, umevujwa baada ya kubainika kuwa na upungufu wa kisheria.

Agosti 22 mwaka jana, Kamishna Andengenye aliingia makubaliano na Kampuni ya Rom Solutions Co. LTD kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya jeshi hilo wenye thamani ya Euro 408,416,238.16 (zaidi ya Sh. trilioni moja).

Hata hivyo, serikali imelazimika kuuvunja baada ya kutofuatwa kwa taratibu za kisheria. Miongoni mwa dosari zilizobainika ni Kamishna huyo kutokuwa na mamlaka kisheria kuingia mkataba huo.

Akitangaza kuvunjwa kwa mkataba huo kwa waandishi wa habari jijini hapa jana, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alisema serikali iliamua kuvunja makubaliano hayo Februari 12 mwaka huu baada ya kupitia mkataba huo.

Alisema baada ya kuupitia mkataba huo, ilibainika aliyekuwa Kamishna wa jeshi hilo hakuwa na sifa ya kuingia mkataba huo.

"Napenda kuujulisha umma kuwa makubaliano yaliyokuwapo awali baina ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Kampuni ya Rom hayapo na yalikwishavunjwa na pande zote kuridhia kuvunjika kwake,"alisema.

Waziri Simbachawene alisema mkataba huo ulikuwa mkubwa na hivyo kamishna huyo hakuwa na sifa ya kuuingia kwa mujibu wa Sheria ya Misaada, Mikopo na Dhamana ambayo inasema mwenye uwezo wa kuingia makubaliano ni Waziri wa Fedha.

"Sasa, hapa kamishna aliingia mkataba, lakini hakuwa na sifa ya kuingia mkataba, hivyo kulikuwa na kuvunja sheria ya nchi, lakini hata upande wa pili na wao ni kama vile yule aliyekuwa anakuja kuingia mkataba, hakuwa na mamlaka ya kisheria ya kuingia mkataba, hivyo pande zote kulikuwa na 'mistakes' (makosa),"alisema.

Simbachawene alisema kutokana na hali hiyo, serikali iliona utasababisha hasara kubwa kwa Watanzania na utekelezaji wake ulikuwa wa kinadharia.

"Kampuni ya Rom Solution wakaona hoja zilivyo na uzito, wakakubali mkataba uvunjwe na mkataba umevunjika na serikali haiwajibiki kulipa au kudaiwa kitu chochote," alisema.

Simbachawene alisema mi-



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa tatu kulia), akiwa pamoja na wakurugenzi wengine wa Benki hiyo, wakionyesha baadhi ya tuzo, wakati wa uzinduzi wa programu maalumu ya kuwawezesha wanawake, kushika nafasi mbalimbali za uongozi, iliyofanyika , jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dk Mpango ataka ushirikiano Sweden katika uwekezaji

**Na Waandishi Wetu,**

**DODOMA**

SERIKALI imesema kuwa ushirikiano mpya kati ya Tanzania na Sweden unatakiwa kujikita katika biashara na uwekezaji kuliko misaada pekee ili kuisaidia Tanzania kuwa na uchumi endelevu na shirikishi.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema hayo jana jijini hapa alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Sweden nchini, Anders Sjoberg.

Dk. Mpango alisema ushirikiano kati ya nchi hizo unatakiwa kuwa na uhalisia kwa kuisaidia Tanzania kutoendelea na utegemezi na badala yake kuongeza kiwango cha biashara kati ya nchi hizo kwa kuwa kiwango cha sasa bado hakitoshelezi.

"Tanzania imejipanga kuondoa utegemezi kwa kuhakikisha inakuwa na uchumi wa viwanda unaotegemea malighafi za ndani. Lengo hili haliwezi kufikiwa iwapo hakuna rasilimali watu yenye ujuzi, hivyo tunahitaji mafunzo na vifaa hususani kwenye elimu ya ufundi stadi ili kupata watu wenye ujuzi wa kuendesha uchumi wa viwanda utakaoongeza thamani ya bidhaa," alisema.



Dk. Mpango alisema uchumi au maendeleo shirikishi haviwezekani kuacha nyuma sekta ya kilimo ambayo ndiyo chanzo kikubwa cha malighafi za viwandani na inahusisha Watanzania wengi na kwanba katika eneo hilo kuna fursa ya uwekezaji kwenye mbegu bora na dawa.

Pia alisema kuna fursa katika sekta ya uvuvi kwenye maziwa na bahari na kwa sasa zana zinazotumika ni duni na hazikidhi mahitaji, hivyo kuiomba Sweden kuangalia uwekezaji katika maeneo hayo.

Sambamba na hilo, alisisitiza umuhimu wa kuwekeza kwenye rasilimali watu ili kupata wataalamu wabobezi ambao ujuzi wao utakuwa unabadilika kulingana na mabadiliko ya mahitaji, hasa katika sekta za afya, kilimo, uvuvi na ufugaji na ambazo zina mchango mkubwa kiuchumi.

Alisema Tanzania imeendelea kupiga hatua kubwa katika sekta ya afya hasa katika matibabu ya ugonjwa wa moyo. Alisema awali serikali ilikuwa inatumia fedha nyingi kugharamia matibabu nje ya nchi lakini kwa sasa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete inatoa tiba hiyo hapa nchini.

Kutokana na hatua hiyo, alisema msaada unaohitajika ni kuongeza wataalam wabobezi ambao wataongeza kasi ya utoaji huduma hizo kwa wananchi.

Kwa upande wake, Balozi Sjoberg, aliipongeza serikali kwa jitihada zake za maendeleo na akaahidi kuendelea kufanya kazi na serikali kwa kusaidia katika miradi ya maendeleo ikiwamo ya kilimo cha umwagiliaji.

Sweden ilianza kushirikiana na Tanzania miaka ya 1960 na sasa mpango mkakati wa ushirikiano unaotekelezwa ulianza mwaka 2013 na kumalizika mwaka jana katika miradi ya nishati, utafiti, elimu na msaada wa kibajeti.

# Lukuvi awashia moto ma-DED kuhusu ardhi

**Na Mwandishi Wetu, SHINYANGA**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amewataka wakurugenzi wa halmashauri zote mkoani Shinyanga, kuharakisha upimaji ardhi na utoaji hati za umiliki ardhi kwa wananchi ikiwamo mipango miji ili kuongeza mapato ya serikali na kuepukana na ujenzi holela.

Lukuvi aliyasema hayo jana mkoani hapa alipofika kwa lengo la kujionea ofisi mpya zitakazotumiwa na Msajili wa Ardhi pamoja na Kamishina wa Ardhi kutoka Wizara yake ikiwa kuwa na uhakika wa utoaji wa huduma za masuala ya ardhi.

"Kuanzia sasa hakuna mwananchi maskini kusafiri kutoka mkoa mmoja kufuata hati mkoa mwingine. Wizara inaweka ofisi kila mkoa yenye vifaa vya kisasa vitavyosaidia masuala yote ya mipango miji na upimaji ardhi katika kila wilaya bila kulazimika kufuata huduma hizo katika makao makuu ya wizara," alisema.

Waziri Lukuvi alisema mkoa wa Shinyanga una hati 15,000 zilizosajiliwa ambazo nyaraka zake zimehifadhiwa na wizara yake lakini kwa sasa zitaletwa na kuhamishiwa mkoani Shinyanga zikiwamo nyaraka zingine za mipango miji ya Shinyanga zilizokuwapo kabla ya uhuru.

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri kupima ardhi na kumilikisha wananchi ili kutumia kama dhamana ya mikopo benki ili fedha zitakazopatikana ziingie katika mzunguko, hivyo kuchochea maendeleo ya mkoa.

Hatua hiyo, alisema itakuwa muhimu katika kukomesha ujenzi holela na kupanga makazi bora badala ya kuanza kuboresha na kuendeleza miji wakati ujenzi holela ulishaanza.

"Unapowamilikisha watu ardhi unaongeza pato la serikali litokanalo na kodi ya ardhi lakini pia unawawezesha wananchi kutumia hati ya ardhi kupata mikopo ya benki ambayo huchangia kuingiza fedha kwenye mzunguko, hivyo kukuza uchumi wa eneo husika," alisisitiza.

Lukuvi alisema benki nyingi mkoani Shinyanga zina fedha nyingi ambazo hazina wakopaji kutokana na watu kukosa dhamana inayowezesha kukopa huku akionya kuwa kuna baadhi ya wilaya hazijafanya mipango yoyote ya uendelezaji ardhi kwa kipindi cha miaka mitano mpaka sasa.

Kutokana na hali hiyo, alisema wizara yake imeanzisha kila mkoa ofisi ya ardhi yenye vifaa pamoja na wataalamu watakaosaidia kutatua changamoto za ardhi na ofisi hizo zitakuwa na mtaalam wa kila sekta ya ardhi kwa lengo la kuweka huduma karibu na wananchi.

HABARI KITAIFA

# Msomi nguli ataka mjadala Azimio la Arusha

**Na Friday Simbaya, MUFINDI**

MWANATAALUMA wa Chuo Kikuu cha Katoliki Ruaha (Rucu), Profesa Gaudens Mpangala, amesema ili kumuezi kwa vitendo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, lazima kuwapo mjadala wa kitaifa wa kujadili Azimio la Arusha.

Prof. Mpangala alisema hayo jana wakati wa mhadhara wa uwasilishaji wa kitabu uliokwenda sambamba na uzinduzi wa Kitabu cha "Mwalimu Kambarage Julius Nyerere na Maedeleo" kilichoandikwa kwa ushirikiano wa wanataaluma wa Rucu, akiwamo Prof. Mpangala mwenyewe. Wengine ni Padri Pius Mgeni, Stephen Kilasi na Claudis Sabuni.

Uzinduzi huo ulifanyika katika Parokia ya Nyololo, Mufundi, Jimbo Katoliki la Iringa na Paroko wa parokia hiyo, Mariano Passmonte.

Alisema ni wakati muafaka kufanya hivyo kutokana na matatizo ambayo Tanzania inapambana nayo kama vile kukua kwa umaskini kwa wananchi walio wengi hasa wa vijijini, kukua kwa pengo la matajiri wachache na maskini wengi, kuporwa kwa rasilimali zake na nchi za mabepari, uchumi wake unataliwa kutoka nje.

Prof. Mpangala aliongeza kuwa Azimio la Arusha ndilo litakuwa itikadi na dira ya taifa bila kujali utofauti wa vyama vya siasa.

Alisema pamoja na nchi kufuata mfumo wa kibepari, kuna mambo mazuri yaliyomo kwenye Azimio la Arusha ya mfumo wa kisoshalisti ili kupata sera nzuri.

Mwanazuoni huyo alisema kuwa kwenye Azimio la Arusha kuna mambo mengi mazuri na kuomba kurudi katika azimio hilo lakini lazima kuwapo mjadala wa kitaifa ili lifanyiwe marekebisho kuendana na mazingira ya sasa.

Alitoa mfano wa China kuwa taifa kubwa kiuchumi duniani ikitanguliwa na Marekeni ni kwamba ilifanya mabadiliko kutoka ndani si kwa msukomo ya nchi za nje kwa kuangalia mambo mazuri yaliyokuwa kwenye mfumo wao wa kisoshalisti na kuyaingiza kwenye mfumo wa kibepari na hatimaye kuibuka na sera ya kuendesha uchumi wake.

Mpangala alifafanua kuwa kuna aina mbili ya ubepari, yaani ubepari uliokomaa na ubepari uchwara na kuongeza kuwa ubepari ulikomaa ni ule unaopatikana katika nchi za kaskazini na ubepari uchwara in ule unaofanywa na nchi maskini za Afrika.

Kwa mujibu wa Prof. Mpangala, mfumo wa sasa hauna nafasi ya kupunguza pengo la walionacho na wasio nacho na matokeo yake ni kuwapo na matabaka katika jamii na kusababisha ubaguzi katika utoaji wa huduma za kijamii katika sekta za afya na elimu na huduma zingine za kijamii.

Baadhi ya watu waliohudhuria hafla hiyo, walisema Mwalimu Nyerere alikuwa na uongozi imara kwa Tanganyika na baadaye Tanzania.

Walisema uimara wa uongozi wake ulijidhihirisha katika mambo matatu ambayo ni itikadi iliyokuwabalika na wananchi wote ya ujamaa na kujitegemea kwa njia ya Azimio la Arusha; msisitizo wake wa umoja wa kitaifa na hali ya amani.

Jambo la tatu kwa mujibu wa watu hao ni maisha ya Mwalimu Nyerere ya juhudi ya kuchapa kazi, kumcha Mungu na kuishi maisha ya kawaida kabisa.



Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP), Simon Sirro, akizungumza na Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika (SADC), Dk. Stergomena Tax, aliyemtembelea ofisini kwake Makao Makuu Ndogo ya Jeshi hilo jijini Dar es Salaam jana na kujadiliana masuala mbalimbali ya kiutendaji. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Laini milioni 36 zasajiliwa rasmi

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA), imesema hadi Machi 10 mwaka huu, laini za simu zilizosajiliwa kwa alama za vidole ni milioni 35.8, sawa na asilimia 83.1 ya laini milioni 43.07 zilizounganishwa mtandaoni.

Mkurugenzi wa TCRA, James Kilaba, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu Siku ya Maadhimisho ya Haki ya Mlaji inayoadhimishwa Machi 15 ya kila mwaka.

"Wakati tunaadhimisha siku hii, ni muhimu tukakumbushana wajibu wa kila mmoja wetu kusajili laini yake ya simu kwa mfumo wa baiometria kutumia kitambulisho cha Nida," alisema.

Alisema kazi ya usajili ni endelevu na wanaendelea kusajili wateja wapya na kuwafungia wale ambao bado hawajisajili kwa alama za vidole.

Alisema lengo la usajili kwa kutumia mfumo huo ni kuimarisha usalama katika matumizi ya simu za mkononi, kulinda watumiaji na kufanikisha shughuli nyingine za usimamizi.

Sambamba na hilo, alisema huduma za kifedha ni miongoni mwa manufaa makubwa ya ukuaji wa teknolojia na sekta ya mawasiliano, akibainisha kuwa takriban Sh. trilioni 5.8 zipo kwenye mzunguko kupitia miamala ya simu.

"Miamala hiyo ya kifedha, imeiweka Tanzania kuwa miongoni kwa nchi ambazo upatikanaji wa huduma za fedha kwa haraka na wepesi kuwa suala linalowezekana.

"Nchi yetu imekuwa ikitolewa mfano linapokuja suala ka ubadilishanaji miamala ya kifedha kwa njia ya simu na tumefanikiwa katika hili," alisema.

Kuhusu Siku ya Haki ya Mlaji, Kilaba alisema usimamizi madhubuti wa huduma za mawasiliano umewezesha wananchi kupata huduma mtambuka za kijamii pasipo kulazimika kunyanyua miguu kama vile elimu kwa njia ya mtandaoni, huduma za fedha, biashara mtandaoni na afya.

# Serikali yapata fedha ujenzi Uwanja wa Ndege Msalato

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imepokea mkopo wa Sh. trilioni 1.14 kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitatu ya maendeleo ukiwamo ujenzi wa Uwanja wa Ndege Msalato jijini Dodoma.

Akizungumza katika hafla ya kutia saini mkopo huo jijini Dar es Saalam jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, alisema kati ya fedha hizo, Dola za Marekani milioni 271.63 zitatumika kujenga Uwanja wa Ndege wa Msalato.

Alisema Dola za Marekani milioni 168.76 ni kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Barabara ya Bagamoyo-Horohoro/Lungalunga- Malindi kwa kiwango cha lami.

James alisema kiasi kingine cha Dola za Marekani milioni 55.2 ni kwa ajili ya programu ya utawala bora na kuendeleza sekta binafsi.

"Kusainiwa kwa mikataba hii kutaiwezesha AfDB kuipatia serikali mikopo ya masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 198.63 kupitia Dirisha la Maendeleo la AfDB, Dola za Marekani milioni 246.96 pamoja na Dola za Marekani milioni 50 kupitia mfuko wa serikali ya China unaosimamiwa na AfDB," alisema.

Aliongeza kuwa utiaji saini wa mikataba hiyo utaongeza kiasi cha fedha ambacho kimetengwa na benki kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa miundombinu ya uchukuzi kutoka Dola za Marekani bilioni 1.03 hadi Dola za Marekani bilioni 1.47, hivyo kuifanya sekta ya uchukuzi kunufaika na asilimia 70 ya misaada na mikopo kutoka AfDB kwa serikali yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 2.1.

Alisema ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Msalato na ujenzi wa kipande cha Barabara ya Bagamoyo-Pangani kwa kiwango cha lami utasaidia serikali kuziba pengo la miundombinu na kuchochea kasi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kupunguza umasikini na kuongeza utalii.

"Utekelezaji wa miradi hii utaimarisha shughuli za uchukuzi na utaongeza faida za mtangamano wa Tanzania kikanda pamoja na mataifa mengine," alisema.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Patrick Mfugale, alisema gharama za ujenzi wa Daraja la Pangani ni Sh. bilioni 448 na serikali itachangia Sh. bilioni 58.473.

Alisema Sh. bilioni 10.3 zimetengwa kwa ajili ya kuwalipa fidia wakazi watakaoathirika na mradi huo na ujenzi wake utachukua miaka mitatu kukamilika.

"Uwanja wa Ndege wa Msalato utakuwa na uwezo wa kupokea ndege aina ya Dreamliner 17, ndege aina ya Airbus 380, Sh. bilioni 15.42 zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia," alisema.

Mwakikishi Mkazi wa AfDB Tanzania, Dk. Alex Mubiru, alisema mikataba hiyo mitatu inaakisi Mpango wa Taifa wa Tanzania kuanzia mwaka 2020-2025.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji Stars oneni thamani ya jezi ya Taifa

TAYARI wachezaji wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars wameingia kambini kujiwinda na mechi za kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021, pamoja na fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.

Kuelekea maandalizi ya michuano hiyo, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Mrundi Etienne Ndayiragiji ameita kikosi cha wachezaji 35 kutoka ndani na nje ya nchi watakaohakikisha wanaipeperusha vema bendera ya Tanzania katika mechi hizo.

Wachezaji wengi wanaocheza soka la ndani tayari wamejiunga na kikosi hicho isipokuwa wale wanaotoka klabu ya Yanga na Namungo wenyewe watajiunga na timu hiyo baada ya mechi yao ya Ligi Kuu Bara hapo kesho katika Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi.

Miongoni mwa wachezaji walioitwa katika kikosi hicho cha Ndayiragije, ni mara ya kwanza kwao kuitwa kuitumikia Taifa Stars, hivyo wanajukumu kubwa la kumdhihirishia kocha huyo kuwa hakufanya makosa kuwapa jukumu la kwenda kuipeperusha bendera ya Tanzania kimataifa.

Lakini pia, jukumu hilo linapaswa kubebwa na wachezaji wote waliopewa dhamana hiyo na Ndayiragije ili kudhihirisha Tanzania ina vipaji vingi katika soka na haikubahatisha kufuzu CHAN pamoja na fainali zilizopita za Afcon nchini Misri.

Tunasema hivyo kutokana na ukweli kwamba licha ya kufuzu kwa mbinde Afcon nchini Misri, Taifa Stars haikufanya vizuri kwenye fainali hizo wakati ikishiriki kwa mara ya kwanza tangu 1980, hivyo ni jukumu la wachezaji kuidhihirishia Afrika na dunia kwa ujumla kwamba kipindi hiki imejipanga upya kuwashangaza wote waliokuwa wakiibeza.

Si Afcon pekee, lakini pia tunakumbuka Taifa Stars ilivyofuzu na kushiriki michuano ya CHAN kwa mara ya kwanza fainali hizo zilipofanyika nchini Ivory Coast kuanzia Februari 22 hadi Machi 8, 2009, haikufanya vizuri, hivyo ni jukumu sasa la wachezaji watakaopata nafasi ya kucheza kutambua thamani ya kuvaa jezi ya timu hiyo ya taifa.

Tunataka kuona kila mchezaji akijitoa kwa kila kitu uwanjani kwa kuanza na mechi ya kuwania kufuzu Afcon ugenini dhidi ya Tunisia hapo Machi 27, mwaka huu kabla ya kurudiana siku tatu baadaye katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Tunatambua haitakuwa mechi rahisi hasa tukizingatia Tunisia ni miongoni mwa timu bora si Afrika pekee bali duniani kwa ujumla, hii ikiwa ni kutokana na kushika nafasi ya 27 katika viwango vya ubora vya Fifa ukilinganisha na Tanzania ambayo ipo nafasi ya 134 kwa sasa.

Lakini hilo haliwezi kututisha hasa tukizingatia Taifa Stars inaingia kambini mapema kujiwinda na mchezo huo huku tukiamini Ndayiragije anajua kuzichanga vema karata zake kulingana na aina ya mpinzani anayekwenda kukutana naye.

Kadhalika, ingawa wengi wanaamini katika michuano ya CHAN itakayoanza kutimua vumbi nchini Cameroon kuanzia Aprili 4-25, mwaka huu, kuwa Tanzania iliyopangwa Kundi D sambamba na Guinea, Namibia na Zambia, ipo kundi jepesi, hatuamini katika hilo.


Tunachoamini Nipashe, wepesi wa kundi hilo utatokana tu namna wachezaji watakavyoweza kujituma kuanzia sasa wakiwa kambini kwa kufuata maelekezo ya kocha na kujiongeza kimazoezi, lakini pia kuona thamani ya kuivaa jezi ya Taifa Stars watakapokuwa katika michuano hiyo, hivyo ni wakati sasa kwa kila mchezaji kulitambua hilo na kulifanyia kazi.

Tunaamini kama kila mchezaji akilitambua hilo, Taifa Stars itakwenda kufuta aibu iliyoipata katika michuano ya Afcon nchini Misri na katika fainali za CHAN iliposhiriki kwa mara ya kwanza mwaka 2009.

Tunataka kuona heshima hiyo ikijengeka ili kuwavutia mawakala wengi kuja kusaka vipaji nchini, na wenye jukumu la kuwaleta ama kuwafanya kuigeuzia Tanzania kisogo, si wengine bali ni wachezaji walioitwa kuitumikia Taifa Stars kwenye michuano ya kuwania kufuzu Afcon na watakaokwenda fainali za CHAN.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Upendeleo unaharibu kandanda

Na Barnabas Maro

UPENDELEO au upendeleaji ni tabia ya kufanya jambo kwa kumili* (*kitendo cha kitu au mtu kuelemea upande mmoja kimawazo au kimatendo; elemea.) Hali ilivyo sasa nchini, upendeleo unasambaa bila kificho kutoka kwenye siasa mpaka michezoni! Tanzania yaelekezwa wapi?

Baadhi ya marefa/waamuzi wa mchezo wa mpira wa miguu, yaani kandanda au kabumbu wanatia shaka uchezeshaji wao hasa wanapokuwa waamuzi wa timu zinazopambana na Simba au Yanga. Wakati mwingine hata timu hizo mbili nazo hulalamikia uamuzi unaotolewa uwanjani. Kongole kwa runinga ya Azam inayoonesha na kurudia mara kadhaa makosa yanayotendeka uwanjani, lakini 'kutoonekana' na waamuzi wanaochezesha mechi hizo!

Je, waamuzi wanaochezesha kwa upendeleo ni mashabiki au wanachama kindakindaki (halisi) wa timu hizo ndo sababu ya kuchezesha kwa kutotumia haki? Kama sivyo, huchezesha mechi hizo kwa kuahidiwa hela? Wahenga walikuwa sahihi waliposema "Fedha fedheha" wakiwa na maana pesa huweza kuleta mambo ya aibu baina ya wanadamu. Methali hii hutumiwa kutuonya dhidi ya maovu yanayoweza kusababishwa na pesa.

Pia walisema "Fedha ilivunja nguu, milima ikalala." Maana yake pesa zina uwezo wa kuvunja vilima na milima. Hii ni methali ya kupigia mfano uwezo wa fedha. Kwamba mtu akiwa na pesa huweza kufanikiwa kufanya mambo ambayo asingeweza kuyafanya wala kudhania kuyafanya.

Maana ya 'kweli' ni uimara wa hoja, bila kutetemeka; udhahiri, waziwazi, bila kusema uwongo. Bao lililofungwa na timu ya Polisi Tanzania dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika mjini Moshi lilikuwa halali, lakini mwamuzi/refa akalikataa!

Dakika tano baada ya bao lile halali kukataliwa na mwamuzi, timu ya Polisi ikapiga mpira wa kona kuelekea Yanga na kuingia kimiani bila wasiwasi na kuwa bao la kusawazisha. Uwanja ukarindima kwa furaha na kedi (mambo yanayoudhi; makuu, majivuno, kiburi): "Kataeni na hilo, kataeni na hilo ..."

Ndo maana wahenga walisema "Mungu hamfichi mnafiki." Maana yake Mungu humfichua mtu mwenye tabia ya uongo na udanganyifu. Methali hii huweza kutumiwa kwa mtu mwenye tabia ya udanganyifu au hila anayedhania kwamba watu hawawezi kuzitambua.

Tuje kwa wapinzani wetu wa Msimbazi, Klabu ya Simba. Nasita kuwaita 'watani' kwani mambo yafanywayo na klabu hizo si utani bali ni uhasama. 'Watani' ni watu ambao aghalabu ni wa makabila tofauti au marafiki wakubwa ambao wameruhusiwa kudhihakiana kwa mujibu wa mila zao pasi na anayetaniwa kukasirika. Kwa ufupi, watani hawadhuriani bali hushirikiana na kusaidiana.

Kwa kuwa mambo hayo hayamo kwa Yanga na Simba, huo si utani bali ni chuki. Hata wahenga walisema "Chuki humchoma anayeihifadhi." Maana yake chuki humsumbua anayeiweka au kuihifadhi. Methali hii yatufunza umuhimu wa kutoiweka chuki kwa kuwa tunajidhuru wenyewe.

Tuirejelee mechi ya Simba na Azam. Kumbuka mpira uliookolewa na mchezaji wa Simba nje ya msitari, na kusababisha bao la Simba, lakini mwamuzi akalikubali!

Katika mechi ya Yanga na Simba iliyomalizika kwa Yanga kushinda bao 1-0, mchezaji wa Yanga, 'Fei Toto' alichezewa rafu mbaya sana ambayo ingeweza kumvunja mguu, lakini 'eti' mwamuzi hakuiona rafu ile! Mungu ndiye aliyemnusuru vinginevyo 'Fei Toto' angekuwa kafungwa plasta ngumu na asingecheza kwa muda mrefu. Aliyemfanyia rafu ile alimwomba radhi gazetini.

Msemaji wa Simba, Haji Manara aliandika mtandaoni kabla ya mechi ya Yanga na Simba: "Wakitoka, (yaani Yanga kutofungwa) narudi Afrika kwa miguu kutoka Ulaya!" Aliyasema hayo akiwa Hispania ambako ili ufike huko au kurudi Tanzania lazima usafiri kwa ndege au meli lakini yeye alisema angerudi kwa miguu!

Kwa maneno hayo maana yake aliidharau sana Yanga kuwa kamwe isingeifunga Simba, lakini mambo yakawa tofauti. Badala yake akasifu jinsi Yanga ilivyoutawala mchezo ule!

"Maneno ni daraja, hayazuii maji kuteremka." Maana yake daraja haliwezi kuyazuia maji ya mto yasiteremke. Maneno nayo hayawezi kumzuia mtu kufanya jambo aliloazimia.

Methali hii yaweza kutumiwa kumnasihi mtu aliyeazimia kufanya jambo fulani asikate tamaa au asivunjwe na maneno ya watu ambayo hayamdhuru kwa namna yoyote. Huweza pia kutumiwa na mtu aliyeazimia kufanya jambo fulani kujitetea dhidi ya maneno ya binadamu.

Tunamsubiri Haji Manara atakayerudi Tanzania kwa 'miguu' kutoka Hispania. Atavuka bahari kwa miguu, kisha akanyage kiguu na njia mpaka Dar es Salaam, Tanzania!

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI KITAIFA

# Jela maisha kwa kubaka, Kulawiti mtoto wa kambo

**Na Daniel Limbe, CHATO**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Chato mkoani Geita, imemhukumu kifungo cha maisha jela, Kazimili Dotto, mkazi wa kijiji na Kata ya Makurugusi wilayani hapa baada ya kupatikana na hatia ya kubaka na kulawiti mtoto wake wa kambo.

Hukumu hiyo imetolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Odira Amworo, baada ya kukamilika kwa maelezo ya pande zote mbili.

Awali, mwendesha mashitaka wa serikali, Anosisye Erasto, akishirikiana na mwendesha mashitaka wa polisi, Mauzi Lyawatwa, walidai mahakamani kuwa mshtakiwa alimbaka na kumlawiti mtoto wa mkewe (mtoto wa kufikia) mwenye umri wa miaka tisa huku akitishia kumuua kwa kisu iwapo angebainisha kutendewa ukatili huo.

Walidai kuwa mshtakiwa alitenda kosa la kwanza la kufanya mapenzi na mtoto chini ya miaka 10 jambo ambalo ni kinyume cha kifungu cha 130 (1) (2) (a) na 131 (3) cha Sheria ya Makosa ya Jinai.

Pia walidai kuwa alitenda kosa la pili ambalo ni kulawiti, kinyume cha kifungu cha 154(1)(a) pamoja na 154(2) cha Sheria ya Makosa ya Jinai sura ya 16 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Ilidaiwa Februari 17, mwaka huu, majira ya mchana, mshtakiwa akiwa nyumbani kwake, alimwita mtoto huyo na kumwomba amletee maji ya kunywa ndani ya chumba anacholala pamoja na mkewe, kabla ya kumbaka na kumlawiti.

Baada ya mtoto huyo (jina tunalo) kufikisha maji, ilidaiwa kuwa alikamatwa kwa nguvu na kumtupia kitandani na baba yake kisha kumvua nguo za ndani na kuanza kumbaka na kumlawiti kinyume cha maumbile.

Wakati hayo yakifanyika, ilidaiwa mama wa mtoto alikuwa shambani na aliporejea alisukuma mlango wa chumba chake uliokuwa umeegeshwa, kisha kumfumania mumewe akiwa kifuani kwa mtoto wao akifanya naye mapenzi huku wote wakiwa uchi.

Ilidaiwa kuwa hali hiyo ilimlazimu mama huyo kupiga yowe kuomba msaada andipo majirani walipofika na kujionea wawili hao wakiwa bado uchi kabla ya kumjulisha polisi kata ambaye alifika na kumweka mshtakiwa chini ya ulinzi.

Baada ya maelezo hayo pamoja na ushahidi wa vipimo vya kitabibu kutolewa kisha upande wa utetezi kuwasilisha utetezi, mahakama ilisema imejiridhisha pasipo shaka kuwa mshtakiwa anayo hatia kwa makosa yote mawili na kumtaka kutumia fursa ya kuiomba mahakama kumpunguzia adhabu.

Hata hivyo mshitakiwa huyo aliiomba mahakama hiyo kumpunguzia adhabu lakini ilikataa maombi hayo na kumhukumu kifungo cha maisha jela ili liwe fundisho kwa watu wengine wenye kufanya vitendo hivyo vya kikatili dhidi ya watoto walio chini ya miaka 10.




Meneja wa Bidhaa za Intaneti wa Tigo, Mkumbo Muyonga, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa simu aina Samsung S20. Kulia ni Meneja wa Samsung Tanzania, Suleiman Mohamed. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RAS awapongeza TCRA elimu uhalifu mtandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Kagera, Profesa Faustine Kamuzora, ameipongeza Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) kwa kuanzisha Kampeni ya Sirubuniki Mjanja Haingizwi Chaka yenye lengo la kutoa elimu ya uhalifu wa mitandao kwa viongozi wa dini.

Alitoa pongezi hizo juzi alipofungua semina ya Kamati ya Amani Mkoa wa Kagera iliyoandaliwa na TCRA ili kutoa elimu ya kujikinga na uhalifu kwa watu wanaotumia huduma za mawasiliano.

"Nawaomba viongozi wa dini muiunge mkono serikali kupitia TCRA kueneza elimu hii kwa waumini wenu na hata ambao siyo ili wafahamu kujikinga na uhaifu wa mawasiliano." alisema.

Alisema viongozi wa dini wana waumini wengi, hivyo ni rahisi kufikisha elimu hiyo na watu wakabadilika kwa kuwa kwa sasa huduma ya mawasiliano inakua kwa kasi kubwa.

"Ninaamini viongozi wa dini mkivalia njuga suala hili, basi watu wataweza kujikinga na uhalifu wakati wanatumia huduma za mawasiliano," alisema.

Mkuu wa Kanda ya Ziwa wa TCRA, Francis Mihayo, alisema viongozi wa dini ni kundi muhimu katika kufikisha ujumbe kwa jamii kwa haraka na kupitia semina hiyo anaamini itazaa matunda kwa wananchi kuwa na uelewa namna ya kutumia mawasiliano.

Aliongeza kuwa kampeni hiyo inalenga kuzifikia kamati za amani za mikoa yote ya Tanzania kwa kuwa kamati hizo ni za viongozi wa dini za madhehebu mbalimbali ambazo zimeundwa kwa lengo la kujenga maridhiano kwa watu wa dini mbalimbali na jamii.

Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa TCRA, Mabel Masasi, alisema katika kutoa elimu hiyo, wanawafikia makundi yote, lengo likiwa ni kulinda usalama wa nchi.

# NIT kuongeza nguvu kiwanda cha magari

**Na Gwamaka Alipipi**

CHUO cha Taifa Cha Usafirishaji (NIT), kimeahidi kutoa msaada wa kiufundi kwa mwekezaji mzawa aliyeanzisha kiwanda cha kuunganisha magari mkoani Pwani.

Kiwanda hicho cha BM Motors kiko Kibaha mkoani Pwani na tayari kimeanza kwa kuunganisha mabasi.

Akizungumza wakati wa ziara ya kutembelea kiwanda hicho juzi, Mkuu wa Chuo cha NIT, Profesa Zacharia Mganilwa, alisema watatoa timu ya wataalamu kutoa msaada wa kiufundi kwa kiwanda hicho kipya cha kuunganisha magari.

Profesa Mganilwa alisema NIT pia itawatuma wahandisi wabobezi katika mitambo, magari na wataalamu wa masoko kuona ni namna gani wataweza kumuunga mkono mwekezaji huyo mzawa kutimiza malengo yake.

"Chuo kitatuma wataalamu wabobezi katika uhandisi wa magari, kila mtaamu ataangalia eneo lake la utaalamu na baada ya hapo wataleta mapendekezo kwa chuo jinsi ya kumsaidia mwekezaji huyo mzawa.

"Kwa mfano, wataalamu wa uhandisi wa magari ambao watatembelea kiwanda hicho cha uunganishwaji wa magari, wataangalia jinsi ambavyo mabasi yatakayokuwa yanaunganishwa hapo yawe yenye ubora wa hali ya juu kabisa, na si vinginevyo," alisema.

Prof. Mganilwa alisema baada ya majaribio yote kufanywa, NIT itatoa cheti ili mwekezaji huyo aanze kazi zake mara moja.

"Baada ya kupewa cheti, taasisi zingine za serikali kama vile Mamlaka ya Mapato (TRA) na Shirika la Viwango (TBS) na wao pia watatoa vyeti vyao vya kumruhusu kuanza kazi rasmi," alisema.

Jonas Nyagawa, Mkurugenzi wa Kampuniya BM, ambaye ndiye mwekezaji mzawa aliyeanzisha kiwanda hicho alisema: "Wazo la kuanzisha kampuni lilianza miaka mitano iliyopita.

"Niliamua kuwekeza katika sekta hii miaka mitano ingawa kwa kipindi kile watu wengi wakiwamo viongozi kutoka serikalini hawakunielewa."

Alisema kampuni yake inalenga kuunganisha zaidi ya magari 100 kwa mwaka.

Nyagawa alisema kuagiza basi la abiria nje ya nchi unalipa Sh. milioni 400, lakini likitengenezwa nchini, gharama zitashuka mpaka Sh. milioni 300.

# Watenga maeneo kudhibiti Corona

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA MJINI**

MKOA wa Shinyanga umeshaunda timu ya wataalamu na kutenga maeneo maalum ya kukabiliana na mlipuko wa virusi vya Corona endapo kutabainika watu kuambukizwa virusi hivyo.

Imeelezwa kuwa hatua hizo zimechukuliwa kutokana na mkoa huo kuwa na viwanda vingi vinavyoendeshwa na wawekezaji kutoka China na migodi ya madini yenye mwingiliano mkubwa wa wenyeji na wageni kutoka nje ya mipaka ya Tanzania.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Nuru Mpuya, alibainisha hatua hizo juzi, alipokuwa mgeni rasmi kwenye kikao cha Baraza la Wazee Mkoa wa Shinyanga pamoja na kikao cha Kamati ya Ushauri ya Watu Wenye Ulemavu mkoani humo.

Alisema Mkoa wa Shinyanga tayari umechukua hatua ya kukabiliana na virusi hivyo, akibainisha kuwa kuna timu ya wataalamu imeshaundwa ambao watashughulika na wagonjwa wenye virusi hivyo na kumetengwa maeneo ya kutolewa huduma kwa wagonjwa hao katika halmashauri zote sita za mkoa huo.

"Serikali mkoani Shinyanga tumeshachukua tahadhari ya kukabiliana na Virusi vya Corona, tumeshaunda timu ya wataalamu na kutenga maeneo ya kutolea huduma wagonjwa watakaopatikana na virusi hivyo, pia tumeshawapima wachina wote kwenye viwanda vyao na wapo salama.

"Maeneo ambayo tumeyatenga, kwa Manispaa ya Shinyanga Kituo cha Afya Kambarage, kwa Ushetu Kituo cha Afya Bulungwa, Msalala Kituo cha Afya Bugharama, Shinyanga Vijijini Kituo cha Afya Tinde, Kahama Kituo cha Afya Mwendakulima, Kishapu Kituo cha Afya Kishapu," alisema.

Ofisa Afya kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mussa Makungu, alitaja dalili za ungojwa huo kuwa ni kukohoa mara kwa mara, kupumua kwa shida na homa kali, akiwataka wananchi kuhakikisha wananawa mikono na kutoshikana, na kupiga chafya kwa kujifunika na kitambaa.

Katibu wa Baraza la Wazee Mkoa wa Shinyanga, Anderson Lyimo, aliiomba serikali kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya kuchukua tahadhari ya kujikinga na maambukizo ya virusi hivyo, hasa maeneo ya vijiji, shuleni, vyuo na kanisani ambayo yana desturi ya kushikana mikono.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania mkoani Shinyanga, Richard Mpongo, alisema kuna haja serikali kuweka ulinzi wa kutosha kwenye viwanda vya wachina na kuwapima mara kwa mara akiamini kinga ni bora kuliko tiba.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Butata iliyopo Musoma Vijijini, mkoani Mara, Yohana Dawi (kushoto), akisoma taarifa za maendeleo ya uboreshaji wa miundombinu ya shule hiyo ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, kwenye kikao cha wazazi shuleni hapo, mapema wiki hii. **PICHA: MPIGA PICHA WET**

# Bil. 16/- zahitajika ujenzi wa madarasa

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

HALMASHAURI ya Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa inakabiriwa na upungufu wa vyumba 800 vya madarasa vyenye thamani ya Sh. bilioni 16.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Jacob Mtalitinya, aliyasema hayo jana katika mkutano wake na waandishi wa habari uliokuwa na ajenda ya kubainisha vikwazo vilivyopo katika halmashauri hiyo na mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2016.

Alisema miongoni mwa vikwazo vikubwa ni upungufu mkubwa wa vyumba vya madarasa na umeanzishwa mpango wa kila kijiji kufyatua matofali 100,000 na kuanzisha benki ya matofali yatakayotumika kujenga vyumba vya madarasa.

Alisema mpaka sasa, kuna maboma zaidi ya 50 ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi na kufikia usawa wa madirisha, hivyo kinachosubiriwa ni serikali kuyamalizia na kinahitajika kiasi cha Sh. bilioni 16 wakati makusanyo ya ndani ni Sh. bilioni mbili kwa mwaka.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa katika kipindi hicho, Manispaa ya Sumbawanga imepata fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwamo serikali kuu, mapato ya ndani na wafadhili na kufanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ya barabara ya kiwango cha lami yenye urefu wa Km 11.5.

Alisema halmashauri pia imejenga Kituo cha Afya Katumba, kuboresha Kituo cha Afya Mazwi na miundombinu ya sekta ya elimu kwa kujenga madarasa, miradi yote hiyo ikighatimu Sh. bilioni 32.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri hiyo, Frank Mateni, alisema halmashauri imekuwa ikitoa mikopo isiyokuwa na riba kwa makundi maalum, hivyo kusaidia kuboresha maisha ya wakazi wa halmashauri kupitia mikopo hiyo.

# Bodaboda wapewa elimu rushwa ngono

**Na Khalfan Chusi**

MKURUGENZI wa Asasi ya Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (Wajiki), Janethi Mawinza, amewataka madereva wa pikipiki, maarufu bodaboda, kuwa mstari wa mbele kukemea rushwa ya ngono baada ya nafasi yao ya kazi kutajwa kuwa miongoni mwa kazi zenye ushawishi mkubwa kwa wanafunzi wa kike.

Alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam alipofungua kampeni ya maandamano ya kupinga rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia iliyowashirikisha bodaboda na wadau wengine.

"Leo (jana) tunazindua maandamano ya kupinga rushwa ya ngono katika Kata ya Gongo la Mboto, baada ya kumaliza maandamano haya Wilaya ya kinondoni sasa tumeamua kutumia madereva bodaboda ambao tayari wana elimu juu ya masuala ya rushwa ya ngono ili kuisambaza elimu hiyo na wakazi wa huku Gongo la Mboto," alisema.

Alibainisha kuwa rushwa ya ngono kwa sasa imekithiri lakini suala hilo halijadiliwi sana kutokana na rushwa hiyo kufanyika kwa usiri.

"Sisi sote hapa ni wazazi,. utajisikiaje mtoto wako anavyoombwa rushwa ya ngono au kufanyiwa ukatili wa kijinsia? Ndiyo maana tumeamua kutoa elimu hii mtaa kwa mtaa huku tukishirikiana na madereva bodaboda ambao ndiyo wanakutana sana na matatizo haya hususani wanapoombwa lifti," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema rushwa ya ngono ni kitendo cha mtu mwenye mamlaka kutumia mamlaka yake vibaya kumtaka mwenye uhitaji, amtumie kimwili ili kumtimizia hitaji lake.

"Mambo haya yanafanyika katika sekta nyingi nchini kama vile mahakamani, hospitalini, shuleni na sehemu zote ambazo watoto wamekuwa wakiomba kazi, kwa hiyo niseme tu ukiona mtu anakuomba rushwa ya ngono, usisisite kumtaja au piga simu namba (113), hapo utapata msaada moja kwa moja," alisema.

Ofisa Maendeleo Jamii na Jinsia Halmashauri Manispaa ya Ilala, Bertha Msagasi, aliwashukuru Wajiki kwa kuipeleka elimu hiyo katika kata ya Gongo la Mboto na kusisitiza kuwa suala hilo silo la Wajiki peke yao.

# RC Gambo atoa onyo wavamizi eneo la jeshi

**Na Cynthia Mwilolezi, NGORONGORO**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amewataka wananchi wote wanaoishi karibu na kiteule cha Loliondo cha Jeshi la Wananchi (JWTZ), kutoingiza mifugo ndani ya eneo hilo au kutokufanya shughuli zozote ndani ya eneo hilo.

Gambo alitoa agizo hilo juzi wilayani Ngorongoro alipoweka jiwe la msingi katika kiteule hicho.

"Jeshi limekuja hapa kwa kazi mahususi ya kulinda mipaka ya nchi yetu na kudhibiti vitendo vya watu wenye nia ovu. Kwa sababu hii, ni marufuku kwa mwananchi yeyote wa Wilaya ya Ngorongoro kuingiza mifugo ndani ya eneo hili au kujenga nyumba za kuishi karibu na eneo la jeshi," alisema.

Alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Rashid Mfaume, kutoa elimu kwa wananchi kuondoka ndani ya eneo la jeshi na karibu na eneo la jeshi.

Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Dk. Freddy Manongi, alisema kiteule hicho kina umuhimu mkubwa kwa kuwa usalama ni muhimu kwa biashara ya utalii.

Alisema kwa kuzingatia umuhimu huo, mamlaka hiyo imetoa kiasi cha Sh. milioni 400 ili kusaidia ujenzi wa kiteule hicho.

"Bila nchi kuwa na usalama wa kutosha, hatuwezi kufanya biashara ya utalii na katika eneo la Loliondo watalii wamekuwa wakiporwa mali zao mara kwa mara, lakini tunaamini kuanzia sasa vitendo hivyo vitakoma kutoka na uwapo wa jeshi katika eneo hili," alisema.

Kamishna wa Uhifadhi wa Hifadhi za Taifa (Tanapa), Allan Kijazi, aliomba kupewa makisio ya umaliziaji wa ujenzi wa kiteule hicho pamoja na vikwazo vinavyokabili kituo hicho ili kitakapokapofunguliwa kisiwe na matatizo yoyote.

Awali, Msimamizi Mkuu wa Ujenzi wa Kiteule hicho, Kapteni Fadhili Mbulu kutoka JWTZ, alisema ujenzi wa majengo manane ya kudumu kwa ajili ya maofisa na askari wa kiteule hicho unaendelea kwa ufadhili wa Tanapa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Alisema vikwazo vinavyowakabili katika kiteule hicho ni upatikanaji wa maji, barabara za ndani ya kambi, barabara kuu inayoingia kambini na kutoka, jengo la mawasiliano, jengo la huduma ya kwanza pamoja na minara ya ulinzi.




Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Avemaria Semakafu (wa pili kushoto), akisikiliza mpango mkakati wa shirika la World Education Initiative (WEI), uliokuwa ukielezwa na ofisa wa WEI, Grace Muro (kulia), alipofanya ziara ya kutembelea baadhi ya shule za sekondari wilayani Karatu, mkoani Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mvua yapeleka balaa Mirerani

**Na Mwandishi Wetu, SIMANJIRO**

BAADHI ya nyumba za wakazi wa Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara na ekari 189 za mashamba, zimeingiliwa na maji kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

Mkazi wa Mtaa wa Msikitini, Hamis Hamza, alisema baadhi ya nyumba zimezingirwa na maji hivyo kusababisha hofu kwao.

Hamza alisema maji yaliyosababisha mafuriko hayo yameungana na mvua iliyonyesha kipindi cha vuli na masika.

"Hali yetu siyo nzuri kwani tulijenga nyumba zetu kipindi hakukuwa na hali hii miaka 10 iliyopita na sasa ndiyo tunakutana na matatizo haya," alisema.

Ofisa Kilimo na Mifugo wa Kata ya Endiamtu, Nasoro Nasoro, alisema mafuriko hayo yamesababisha maji kuingia kwenye ekari 189 za mashamba ya eneo hilo.

Nasoro alisema sehemu kubwa ya ekari zilizoingiliwa na maji, mazao yake yameharibika kwa kiwango kikubwa na kukatisha tamaa wakulima.

Ofisa Tarafa ya Moipo, Joseph Mtataiko, alisema watu wanaoishi kwenye eneo la mabonde wanapaswa kuondoka kwa kuwa tayari walishafidiwa.

Mtataiko alisema serikali haiwezi kutoa msaada kwa watu wanaoishi kwenye maeneo hayo ya mabondeni kwa kuwa walipewa viwanja na kutakiwa kuondoka.

"Wengine baada ya kufidiwa viwanja waliviuza na kuendelea kukaa kwenye maeneo ambayo kipindi cha mvua kunakuwa na mafuriko, alisema.

## Madiwani wengine wawili Chadema watimkia CCM

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA MJINI**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimeendelea kupoteza viongozi wake jijini Arusha baada ya juzi madiwani wake wawili kujiuzulu nafasi zao na kuhamia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Madiwani hao ni Isaya Doita wa Kata ya Ngarenaro na Damuni Melamari wa Kata ya Sakina, wote wakichukua uamuzi huo kwa madai yaliyowahi kutolewa na wenzao waliohama kwamba kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa jana, Doita alisema kwa muda ametafakari juu ya kukihama chama chake, lakini alikuwa anasita.

"Lakini, sasa moyo umeamua kwa sababu nafsi inanisuta Rais anafanya maendeleo bila ubaguzi. Kata yangu ya Ngarenaro tumejengewa barabara za lami kote na mazingira ya shule za msingi na sekondari yameboreshwa, sasa sioni sababu ya kubaki nje ya mlango, bora niingie ndani ya mlango nikaunge juhudi vizuri," alisema.

Alisema Rais Magufuli kwa kushirikiana na viongozi wake wa Jiji la Arusha, wamefanya mambo makubwa ya kimaendeleo kwa wananchi wa chini.

Alidai haoni sababu kubaki katika chama ambacho haoni dira, bora ajiunge na CCM ambacho kinapigania maendeleo ya wananchi.

Diwani wa Sakina, Damuni, alisema ameona wakati umefika kwake kwenda CCM kuunganisha nguvu kwa ajili ya maendeleo zaidi ya sasa.

"Kweli nimeunga mkono juhudi za Rais Magufuli na nimeona niungane naye ndani tupambane pamoja, hasa katika uchaguzi wa mwaka huu," alisema.

Mpaka sasa madiwani wa Chadema wa kata 19 kati ya 25 za jiji hilo wamejiuzulu na kujiunga na CCM.

Mkurugenzi wa Halmsahauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, alithibitisha kupokea barua za madiwani hao za kujiuzulu.

# Hai yaingizwa mpango upimaji VVU

**Na Godfrey Mushi, HAI**

KATA saba na vijiji vyake vilivyoko pembezoni mwa barabara kuu wilayani Hai, Kilimanjaro, vimeingizwa katika mnyororo wa huduma za upimaji wa virusi vya ukimwi na kuunganishwa na huduma ya dawa za kufubaza virusi hivyo.

Akizungumza jana katika kikao cha wadau wa mradi wa 'shirikisha wote' unaotekelezwa wilayani Hai, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Tanzania Women Research Foundation (Tawref), Dafrosa Itemba, alisema wameamua kujikita kwenye makundi ambayo si rahisi kufikiwa na huduma, wala si rahisi kutafuta huduma za afya kutokana na sababu zao mbalimbali.

"Walengwa watakaoguswa na mradi huu ni wanawake, wasichana wanaoishi maisha hatarishi, wanaume (mapatina/ madereva wa bodaboda na malori), wanaoishi na ulemavu, wanaoishi na VVU na jamii kwa ujumla ili kufikia lengo endelevu la tatu, namba tatu la Milenia (SDG 3.3).

"Nia yetu ni kuwezesha ufikiaji wa haki ya afya, haki ya kupima virusi vya ukimwi na afya ya uzazi kwa wanawake na wasichana walio katika hatari ya maambukizi katika Wilaya ya Hai," alisema.

Mradi huo wa shirikisha wote unatekelezwa na Tawref, kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID) kupitia Shirika la African Initiatives la Uingereza.

Aidha, Katibu Tawala wa Wilaya ya Hai, Upendo Wella, akieleza msimamo wa serikali wilayani humo alisema: "Kupitia mradi wenu huu kuna mambo mengi ambayo mnayafanya, mmeweza kuibua mambo mbalimbali ambayo yanaibuka kwenye jamii, hususani katika suala ambalo tunalizungumza hapa la kuhakikisha kwamba mnatoa elimu ya uzazi na kujitambua kwa mwanamke.

"Kupitia mradi huu tunaamini kuna elimu ambayo mnaitoa na mnasaidia kuikoa jamii ambayo pengine inaweza kujikuta imetumbukia katika mambo ambayo haikutarajia iingie, lakini kutokana na mazingira ambayo yanawazunguka wanajikuta wametumbukia katika mazingira hatarishi.

Zaidi aliongeza: "Sisi kama serikali tuko tayari kutoa ushirikiano mnaouhitaji, niwapongeze watendaji wetu wa kata, inaonyesha kuna namna wanawapa ushirikiano mpaka na ninyi mnaridhika kwa ushirikiano mnaoupata."

Kata zilizoko kwenye mradi huo ni Muungano, Bomang'ombe, Weruweru, Masama Kusini, Mnadani na Bondeni.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Helga Mchomvu, akizungumzia hali ya ukatili wa kijinsia inavyoendelea kuumiza makundi hayo ya wanawake alisema,

"Kwa kweli mmetufariji, mmefanya kazi ambayo inaonekana lakini bado tuna changamoto katika ukatili wa kijinsia, na ukiangalia ukatili wa kijinsia ambao unafanyiwa akina mama, wanafanyiwa watoto wetu lakini kuna ukatili unaofanyika hivi sasa ndani ya nyumba na hatuna idadi wala hesabu, wala alama tunaweza tukazungumza hapa na sijawahi kuvisikia. "Mmebakiza mwaka mmoja wa kutekeleza mradi huu, lakini tunapata kigugumizi, tunaomba tuwasikie mnaendelea wilayani kwetu kutoa elimu."




Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Yohana Sintoo (kushoto), akikabidhi sehemu ya miche ya miti 100, kwa mmoja wa wakuu wa shule za sekondari za wilaya hiyo, mkoani Kilimanjaro, jana, ili kuanza utekelezaji wa mpango wake wa kuibadili Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai kuwa ya kijani. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Soko la madini Same ladoda

**Na Mary Mosha, MOSHI**

SOKO la madini lililofunguliwa na serikali mwaka jana katika Wilaya ya Same, limeshindwa kufanya vizuri kutokana na kukosekana kwa wateja wa vito, madini yanayopatikana katika maeneo hayo.

Imeelezwa kuwa hali imesababisha serikali kuwapa madalali wa madini vibali vya kutafuta wateja.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kilimanjaro, Fatma Kyando, alisema jana kuwa aina nyingi za madini yanayopatikana wilayani Same ni ya vito na kwamba soko lake kubwa liko jijini Dar es salaam na Arusha na hakuna wateja wanaofika kununua hapo.

Alisema kutokana na hali hiyo, ofisi yake imekuwa ikitoa vibali kwa madalali wa madini kuyapeleka Arusha au Dar es Salaam ambako ndipo kwenye wateja wakubwa wa madini ya vito.

''Madini pale ni ya vito na soko liko chini, hivyo ni vigumu kwa mchimbaji kutafuta soko kutokana na umbali ndio maana tukahamua kutoa vibali pale pale ili wale madalali waweze kwenda kutafuta wateja huko wanakopatikana," alisema Kyando.

Pia alisema alisema ofisi yake iko katika hatua za mwisho kufanikisha kufungua soko la madini katika wilaya ya Moshi, lengo likiwa ni kusogeza huduma karibu na wananchi na vile vile kuzuia utoroshaji wa madini nje ya nchi.

Alisema soko hilo ambalo litakuwa la pili kwa mkoa wa Kilimanjaro baada ya lile la Same litatoa wigo mpana kwa wafanyabiashara wa madini na wachimbaji kuweza kuwa na uhakika wa soko na kuondoa viashiria vya utoroshaji madini vitakavyokuwapo.

''Soko litaanza kazi muda si mrefu hivyo badala ya kutoa vibali vya kwenda kutafuta wateja nje ya mkoa jambo hili litaweza kufanyika hapa hapa kwetu na haya ndio maelekezo ya serikali ili kuziba mianya ya upotevu''alisema

John Tesha, ambaye ni sonara katika mji mdogo wa Himo, alisema uwapo wa soko hilo utamwezesha kupata aina mbali mbali za madini ya vito kwa ukaribu tofauti na ilivyo sasa ambapo huyafuata Arusha.

Alisema kufuata madini mbali hupoteza muda na gharama na ara nyingine hukosa uhakika wa upatikanaji wake kutokana na uhitaji kuwa mkubwa na sehemu ya kupatikana ni moja tu.

# Harufu sokoni yakera wadau

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

SOKO la Bomang'ombe, Hai mkoani Kilimanjaro, limekithiri kwa takataka zinazotoa harufu mbaya, hivyo kulalamikiwa na baadhi ya wafanyabiashara kuwa linahatarisha usalama wa afya zao.

Wafanyabiashara hao, wakiwamo wanaomiliki maduka yanayolizunguka soko hilo, waliiambia Nipashe juzi kuwa takataka hizo zinatupwa nje ya soko.

Kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya wafanyabiashara ya mazao ya chakula, Zainab Mohamed na John Mollel, walisema takataka hizo zimerundikwa kwa muda mrefu bila ya kuzolewa na mamlaka zinazohusika.

"Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai inapaswa kuliangalia jambo hili kwa sababu waathirika wa kwanza tutakuwa sisi, hata wafanyabiashara tunahimizana wenyewe ni vyema kuzingatia kanuni za usafi, lakini mrundikano wa uchafu uliopo katika soko hili unawasukuma na wao kujisahau wajibu wao," alisema Mohamed.

Naye Mollel alisema kuwa katika kipindi hiki ambacho mvua zimekuwa zikinyesha mfululizo, wamekuwa wakizishuhudia taka hizo zikioza na hatimaye kutoa harufu mbaya.

Mmoja wa wafanyabiashara ya nyama, Alli Abdallah akizungumzia adha hiyo, alisema: "Uchafu huu una zaidi ya wiki tatu sasa umejaa na haujazolewa, na kila mwezi tunatoa pesa kwa ajili ya uzoaji wa takataka, lakini tunashangaa hauzolewi na inzi sasa hivi wanatoka kwenye uchafu huo wanaingia kwenye biashara zetu, kama unavyoona inzi walivyo kwenye nyama zangu.

"Kila siku tunahimizwa kufanya usafi na tunafanya hivyo, lakini hao wanotakiwa kuzizoa hizo taka na kwenda kuzitupa, ndiyo inakuwa changamoto. Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya ameshapiga kelele sana kuhusu jambo hili la uchafu, lakini linajirudia sijui wanakwama wapi, tunaomba watusaidie kuzoa ili watupunguzie woga wa kufanyabiashara katika soko hili."

ofisa Mazingira wa Wilaya hiyo, Alfred Njegite, alipotafutwa kutoa ufafanuzi kuhusu malalamiko hayo, alisema gari la kubeba taka liko kwenye matengenezo kwa wiki nzima, ndiyo maana kukajitokeza tatizo hilo lakini akaahidi litarejea kufanya kazi hiyo siku chache zijazo.

# Bunge lahofu usalama jengo soko la madini

**Na Augusta Njoji, DODOMA MJINI**

KAMATI ya Bunge ya Nishati na Madini, imeonyesha kutoridhishwa na jengo la soko la madini jijini Dodoma na kuiagiza Wizara ya Madini kutafuta jengo litakalokuwa na usalama na hadhi ya kufanya biashara hiyo.

Vilevile, kamati hiyo imeitaka wizara kuwasilisha mapendekezo ya namna ya kumaliza malalamiko ya wawekezaji kuhusu usumbufu, gharama kubwa na utaratibu mbaya wa kusafirisha nje bidhaa zitokanazo na madini nchini.

Maagizo hayo yalitolewa juzi na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dustan Kitandula, katika ziara ya kamati yake kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa na wizara hiyo.

Alisema jengo linalotumika kama soko la madini kwenye mkoa huo linatia aibu na haliendani na hadhi ya makao makuu ya nchi. "Mtakumbuka masoko haya yalianzishwa bila kuwapo na bajeti ya uanzishwaji wake, jukumu liliachwa kwa mikoa, wapo waliofanya kwa uthubutu mkubwa kwa kujenga, lakini hili la Dodoma linatutia aibu," alilalamika.

Kiongozi huyo wa kamati alisema licha ya kwamba biashara kwenye soko hilo si kubwa, haliwezi kuachwa jinsi lilivyo hivi sasa.

"Hatuwezi kuliacha likatutia aibu, hebu wizara angalieni kwa umuhimu wa Dodoma pamoja na kwamba mambo haya yaliachwa mikononi mwa mikoa, tuangalie namna ya kuondokana na aibu hii, tuwe na eneo zuri la biashara, na waende wakajifunze kwa wengine," alisema.

Akizungumzia usafirishaji, mwenyekiti huyo alisema wawasilishe maelezo kwa kuwa suala hilo limekuwa likisikika mara kwa mara na ni vyema hatua zikachukuliwa. Awali, mjumbe wa kamati hiyo na Mbunge wa Bukoba Mjini, Wilfred Lwakatare (Chadema), alisema ni muhimu kuangaliwa usalama wa soko hilo kutokana na mazingira yake kutoridhisha.

Mjumbe mwingine na Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Msukuma (CCM), alisema soko hilo halina hadhi licha ya mkoa huo kuwa na machimbo machache ya madini.

"Dhahabu haiwezi kukaa sehemu chafu, matajiri wanakuja na mabilioni yao, mtu anakutana na kiti cha plastiki ofisini, jamani tuweke jengo litakalovutia wawekezaji, hata sehemu za kuchomea dhahabu ziangaliwe ili kuwapo na usalama wa watu," alisema.

Waziri wa Madini, Doto Biteko, alisema wizara itatekeleza yote yaliyoshauriwa na kamati ikiwamo uboreshaji soko hilo.

"Tulianzisha masoko kwa haraka kutokana hali ya utoroshaji madini ilikuwa mbaya sana mpaka tunakuja kukamata kilo 300 za madini kwa tukio moja, hali ilikuwa si shwari," alisema.

Biteko alisema serikali itaendelea kuimarisha masoko hayo huku akitolea mfano Soko la Arusha ambalo kwa sasa ni bora na linavutia wawekezaji.

"Jengo hili ni la Mkoa wa Dodoma tutakutana na Katibu Tawala wa Mkoa ili kuliboresha na tutafanya hivyo mapema iwezekanavyo kuanzia leo (jana) tuone tunawezaje kuliboresha jengo hilo na kuwa la kisasa," alisema.

Kaimu ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Dodoma, Laurent Bujashi, alisema kabla ya kuanzishwa kwa soko husika kwa kipindi cha miezi sita, ukusanyaji wa mapato ulikuwa wa jumla ya Sh. milioni 118.4 ikiwa ni wastani wa Sh. milioni 23.6 kwa mwezi.

Bujashi alisema baada ya kuanzishwa kwa soko la madini Mei mwaka jana, makusanyo yaliongezeka hadi kufika Sh. milioni 486.8 kwa kipindi cha miezi sita, ikiwa ni wastani wa Sh. milioni 54.1 kwa mwezi.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (kushoto), akijadiliana jambo na Naibu Waziri wake, Anthony Mavunde, wakati wa vikao vya Kamati za Bunge, vinavyoendelea, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Corona 'yailiza' Wizara ya Maji

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WIZARA ya Maji imesema mlipuko wa Virusi vya Corona umesababisha kukosa ujuzi kutoka kwa wataalamu wa nje ya nchi ambao wamezuiliwa kushiriki katika Wiki ya Maji itakayoadhimishwa kitaifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema hakuna watalaamu kutoka nje watakaoshiriki katika wiki hiyo.

Alisema wiki hiyo itatumika kutathmini mafanikio katika utatuzi wa kero zilizojitokeza katika sekta ya maji katika kipindi cha miaka mitano.

"Kaulimbiu ya mwaka huu ni 'mabadiliko ya tabianchi ni usalama wa maji kwa wote'. Pamoja na kutathmini, pia kuna miradi mbalimbali itazinduliwa," alisema.

Prof. Mkumbo alisema kutakuwa na mkutano wa wataalamu wa maji ambao utajadili mafanikio na kero za sekta hiyo.

Alibainisha katika wiki hiyo, kutakuwa na mkutano kati ya serikali na wadau wa sekta ya maji utakaofanyika Machi 21.

Alizitaka mamlaka kurekebisha mita za maji ili kila mmoja alipe bili stahiki.

"Hakuna sababu ya watu kulalamika kuhusu malipo ya bili, kila mita wataalamu wanapaswa kwenda kurekebisha, nchi yetu imekuwa ikiadhimisha wiki ya maji kila mwaka Machi 16-22," alisema.

# Wastaafu wapewa mbinu kupata fedha

**Na Renatha Msungu, DODOMA MJINI**

MSHAURI Mwelekezi na Mratibu wa Mafunzo Mafupi na Ushauri wa Kitaalamu, Dk. Hassanal Issaya, amewataka wastaafu kubuni miradi ya ujasiriamali ili kujiongezea kipato baada ya kustaafu.

Alitoa rai hiyo juzi katika mafunzo ya ujasiriamali kwa wastaafu watarajiwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yaliyofanyika jijini Dodoma.

Alisema baada ya kustaafu, ni vyema kuangalia mazingira rafiki ya kufanya ujasiriamali na kuwa na mipango ambayo haiwezi kumsababishia mstaafu hasara.

Alisema ili kufanya vizuri katika ujasiriamali, ni lazima kufanya kazi kwa bidii sambamba na kuwa mbunifu katika kufanya shughuli ya kumwingizia kipato.

"Ili uwe mjasiriamali mzuri, ni lazima ufanye kazi kwa bidii na kuwa mbunifu katika kuibua miradi na kuboresha bidhaa ambazo unazipeleka sokoni.

"Tunajua wakati wa utumishi mlikuwa mkifanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu, lakini katika ujasiriamali hakuna sheria za aina hiyo, hivyo ni wewe mwenyewe unayefanya kazi kwa muda uliopanga," alisema.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Remidius Kisanko ambaye ni mkufunzi kutoka Chuo cha Ualimu Sumbawanga, alisema mafunzo hayo yamewafanya kuelewa nini wanachotakiwa kukifanya baada ya kustaafu.

"Tumejifunza mambo ya kujiepusha nayo wakati wa kustaafu, pia tumejua nini kinaweza kusababisha msongo wa mawazo kwa wastaafu," alisema.

Mshiriki mwingine, Hadija Madaha kutoka Wizara ya Elimu makao makuu, alisema amepata faraja kupitia mafunzo hayo hususani katika kipengele cha upandishwaji wa madaraja.

Alisema alianza kazi mwaka 1974, lakini alipandishwa daraja mara moja tu, jambo ambalo lilimuumiza hasa wakati huu ambao anatarajia kustaafu.

Alisema kupitia mafunzo hayo, amejifunza namna ya kuendesha miradi baada ya kustaafu badala ya kujiingiza katika mikopo.

# Wataalamu wazuru kituo cha wagonjwa wa Corona

**Na Rahma Suleiman, UNGUJA**

UJUMBE wa wataalamu wa afya kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, umetembelea jengo la dharura lililotengwa kwa ajili ya matibabu ya wagonjwa watakaogundulika kuwa na virusi vya Corona lililoko Kidimni Wilaya ya Kati Unguja.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Zanzibar, Halima Maulid Salum, alisema serikali imeamua kuwa na tahadhari hiyo kutokana na ugonjwa huo kuingia Afrika.

Alisema hatua hiyo pia imechukuliwa kutokana na Zanzibar kuwa na mwingiliano mkubwa wa wenyeji na wageni kutoka nje ya mipaka ya Tanzania.

"Eneo hili ni maalum lililotengwa kwa kuwahifadhi wagonjwa wataogundulika na ugonjwa huo hatari ambao huambukiza kwa njia ya hewa na kusambaa kwa haraka sana," alisema.

Alisema kwa sasa hakuna mtu yeyote aliyegundulika kuwa na viashiria vya maradhi hayo, hivyo ni vyema kuchukua tahadhari ili kuudhibiti ugonjwa huo.

Profesa Mohamed Bakari, daktari kutoka Tanzania Bara, alisema watashirikiana na Serikali ya Zanzibar katika kutoa huduma na kuudhibiti ugonjwa huo.

Alisema ni lazima kujipanga mapema katika kukabiliana na ugonjwa huo na athari za mlipuko wa virusi vya Corona ambavyo vinasambaa kwa haraka kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine.

Profesa Mohamed alisema serikali zote mbili zimeweka vifaa maalum vya kutambua hali za kiafya za wageni wanaoingia nchini.

Aliwatoa hofu wananchi kuwa Tanzania hadi sasa ipo salama na wageni wote wanaoingia wanakaguliwa ili kulinda afya za wananchi.

Ujumbe huo ulikagua pia Uwanja wa Ndege cha Kimataifa wa Abeid Aman Karume, Bandari ya Zanzibar Malindi pamoja na Jengo la Kurekebisha Tabia lililoko Kidimni.



Ofisa Afya Bandari ya Zanzibar akimfanyia uchunguzi mmoja wa abiria walioshuka Bandarini hapo jana, kutoka Tanzania Bara kuona kama yupo na virusi vya Corona au hapana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Rais Shein asisitiza elimu kwa wasanii

**Na Rahma Suleiman, UNGUJA**

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuchukua hatua za kuimarisha sanaa na kuendeleza utamaduni kwa kuwaendeleza wasanii kitaaluma.

Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, aliyasema hayo alipohutubia mkutano kati yake na wasanii wa Zanzibar kwenye Ukumbi wa Sheikh Idris Abdul Wakil, Kikwajuni kisiwani Unguja.

Alisema jitihada maalum zitachukuliwa kuhakikisha kazi za sanaa zinatoa fursa kubwa zaidi ya ajira kwa vijana kwa kufanya shughuli zao kisasa na bora zaidi ambazo zitatumia fursa ya soko la utalii.

Dk. Shein alisema katika kuyafikia malengo hayo, serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha nyumba ya sanaa iliyoko Mwanakwerekwe kwa kuijenga upya na kuwa na jengo la kisasa lenye taswira nzuri.

Alisema nyumba hiyo itawekwa vifaa vya kisasa na kuongeza walimu wa fani mbalimbali za sanaa na kukamilika kwa hatua hiyo kutatoa nafasi muhimu kwa vijana wa Zanzibar kupata sehemu nzuri ya kujifunza na kupata ujuzi wa fani mbalimbali.

Alisema sanaa na utamaduni ni nyenzo muhimu za kuitambulisha jamii na ni hazina muhimu ya kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kuwa jamii isiyokuwa na utamaduni, mila, silka, desturi pamoja na sanaa yake inakuwa kama vile haipo.

"Nimefurahi sana kukutana na ninyi wasanii kutoka Unguja na Pemba na kueleza kuwa jamii ya watu wa Zanzibar kama zilivyo jamii nyingine duniani nayo pia ina sanaa, tamaduni, mila, silka, desturi zake tangu enzi zilizoachwa na wazee, hivyo ni lazima zitunzwe, zidumishwe na ziendelezwe," alisema.

Rais Shein alisema sanaa imeiletea sifa Zanzibar na kuifanya ijulikane miaka mingi iliyopita na historia inaeleza wasanii wa zamani akiwamo Marehemu Bibi Siti binti Saad tangu miaka ya 1930 aliyeitangaza Zanzibar kwa muziki wa taarabu kiasi cha kufika India na mataifa mengine duniani.

"Sanaa ni uhai wetu, kwa hakika maisha bila ya sanaa yangekuwa chapwa na kama yanauzwa yangekuwa bure... kwa mnasaba huo, kazi za wasanii ni muhimu na nakuhakikishieni kuwa Serikali ya Zanzibar inathamini sana na inatambua umuhimu wa wasanii," alisema.

Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Ali Karume, alisema wizara inachukua hatua mbalimbali kuwaendeleza wasanii wa Unguja na Pemba ikiwa ni pamoja na kuiendeleza lugha ya Kiswahili ili iendelee kuwa lugha ya taifa.

## Aanika fursa vituo mafunzo ya amali

**Na Rahma Suleiman, UNGUJA**

NAIBU Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mohammed Ahmada Salum, amezitaka taasisi za serikali na binafsi, kuvitumia vyuo vya mafunzo ya amali vya serikali vilivyopo kisheria, kupata vifaa zikiwamo sare na samani za ofisini ili kuwaunga mkono katika utendaji wa kazi zao.

Salum aliyasema hayo katika Mnara wa Mapinduz Square Michenzani juzi, alipofungua juma la Mamlaka ya Mafunzo ya Amali.

Alisema kwa kufanya hivyo, kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha kazi za vijana ili kuongeza kasi ya ufanisi na kutambua uwapo wa vituo hivyo.

Alisema wanafunzi wa vyuo hivyo wanafanya kazi nzuri ya kutengeneza vitu mbalimbali ambavyo vitasaidia serikali kukuza uchumi na kufanikisha azma ya serikali kuwa na nchi yenye uchumi wa viwanda.

Alisema Serikali ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, zimedhamiria kuifanya nchi kuwa na uchumi wa viwanda ili kusaidia kuinua kipato cha mwananchi na taifa kwa ujumla.

Alisema Serikal ya Zanzibar imekuwa ikiwahimiza vijana kujiunga na vyuo vya mafunzo ya amali ili kupata wataalamu watakaoanzisha viwanda hivyo na kutengeneza bidhaa zenye ubora zitakazoleta tija nchini.

Alitumia fursa hiyo kuwataka wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao katika vyuo hivyo vilivyoko Unguja na Pemba ili kuwasaidia vijana kupata taaluma itakayowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kuajiri wengine.

Aliwataka vijana kuendelea kufanya kazi kwa uadilifu na uzalendo katika kufikia Zanzibar ya viwanda.

Alisema serikali itaendelea kuviimarisha vituo vya amali ili kutoa fursa kwa vijana kwenda kupata ujuzi wa kujiajiri na kujipatia kipato.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Bakari Ali Silima, aliwataka vijana ambao hawakubahatika kuendelea na masomo, kujiunga na vituo ili kupata ujuzi wa kazi za mikono na kujiajiri au kuajiriwa.

Akisoma risala kwa niaba ya vituo vya mafunzo ya amali, Sabra Khamis Kalam, aliishauri serikali kuviendeleza vituo hivyo ili kuishajihisha jamii juu ya mafunzo hayo ambayo yatasaidia kukuza uchumi wa nchi, kuongeza kipato kwa jamii na kuendeleza viwanda nchini.



KATY HONGERA KUITWA MAMA KIJACHO Soma UK.20

JUMAMOSI MACHI 14, 2020

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI TELE



AMKENI..AMKENI!

# Wastara, Z Anto wameanza tena

BASI SAWA

# WALITAKA NIFE Hawa apasua

MWIMBAJI wa kibao pendwa 'Nitarejea', Hawa imesema kuna wakati baadhi ya watu walitaka apotee duniani wakati akipambana kunusuru maisha yake,

Akizungumza na EATV, Hawa amesema kipindi anaumwa alikuwa anasikia maneno mengi kutoka kwa watu ambao walikuwa wanatamani afe.

Msanii huyo amesema licha ya matatizo yaliyomtokea alijitakia mwenyewe kutokana na unywaji wa pombe, aliambiwa maini yake yameoza na tumbo limejaa maji, kumbe sio kweli, bali lilikuwa tatizo la moyo uliosababisha mishipa kushindwa kufanya kazi.

"Neno pombe limenifanyia kitu kibaya kwenye maisha yangu, japo sasa hivi nipo sawa na naweza nikanywa ila nikikumbuka yaliyonitokea sitamani tena. Tumbo langu lilijaa watu wakasema maini yameoza lakini sio kweli, tatizo lilikuwa ni moyo na mishipa ilikuwa haifanyi kazi vizuri ndiyo maana nikawa najaa maji tumboni" ameeleza.



# Dorah acha kuwavunga watu

MWIGIZAJI kutoka Bongo Muvi, Dorah Official amesema hawezi kumhonga mwanaume gari hata kama mapenzi yamemzidi.

Dorah amesema hayo wakati akizungumzia madai kwamba kamuhonga gari aina ya IST mwanamume.

Amesema mwanaume anayeonekana wakiwa wote kwenye gari hana uhusiano naye wa mapenzi kwani ana mtu wake yupo kijijini.

"Siwezi kumuhonga mtu kwenye maisha yangu, najua nilipotoka, ninapoelekea na ninachokifanya kwanza mama yangu ana mambo mengi yanamzonga na matatizo ya familia yangu yaniumiza kichwa halafu nimhonge mwanaume IST haiwezi kutokea" , ameeleza Dorah.





# Mh! We Makabila eti hupendagi kitonga?

MWANAMUZIKI wa singeli, Dulla Makabila, amepinga maneno ya watu kwamba yeye anapenda kulelewa na wanawake, badala yake ana bahati ya kupendwa na wanawake wenye vipato vikubwa.

Makabila amesema binafsi hapendi wanawake wasio na vipato kwa sababu yeye mwenyewe bado anatafuta pesa.

"Mimi sio mtu wa dizaini ya marioo au king'asti, natafuta pesa zangu mwenyewe, ila ni mtu ambaye nina bahati ya kupendwa na wanawake ambao wapo vizuri kimaisha sio kwamba ndiyo ninaowatafuta " Dulla Makabila.

Aidha msanii huyo ameongeza kwa kusema "Pia ninampenda mwanamke mwenye kipato na hata asingekuwa na kipato bado ningempenda tu".

## INSTA-TWITTER





**Pambana** ungali una nguvu nguvu, zikiisha mapambano hutayaweza tena- **Shilole.**



**Mkemia** mkuu katika kiwanda cha kuonja pombe anaitwa Masele cha pombe. Maoni kwake- **Kiwewe.**



# Nandy ashangaa mauzauza

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Nandy, ameelezea wasiwasi wake kuchezewa mchezo mchafu baada ya kuona miujiza katika mtandao wa Youtube ambako video ya wimbo wake mpya 'Na Nusu' ametambulisha.

Nandy amesema kwa siku nne ameshuhudia mauzauza baada ya idadi ya watazamaji kupungua, licha ya siku moja kabla ilikuwa ya juu.

Akitoa taarifa hiyo kupitia ukurasa wake wa Instagram, amesema anafanyiwa vitu vya ajabu na watu asiowajua ambao wanamrudisha nyuma kwani nusu ya idadi ya watazamaji wanapungua.

"Nimevumilia hii siku ya nne sasa, huko Youtube kunatokea vitu vya ajabu sana sijui nini tatizo, ikifikisha watazamaji laki tisa, wanarudishwa nyuma hadi laki nane au saba, naona miujiza tu kwenye akaunti yangu, sitaki kuhukumu watu naomba watu wa ufundi wanisaidie kujua kuna nini" ameandika Nandy.

## UNASEMAAA...

# Jitu Baya 'Kimewaka' mashabiki watafutana

RAPA anayechipukia, Jitu Baya, ameangusha singo yake ya pili inayoitwa 'Kimewaka' na kutamba kasi yake haitapungua.

Miezi miwili iliyopita msanii huyo alitambulisha wimbo wake 'Flow Kali' ambayo ilifanya vizuri kwa mashabiki wa muziki nchini.

Akizungumza na BT jana, rapa huyo ambaye sauti yake anafanana na Chidi Benz, amesema wimbo huo umerekodiwa katika studio ya Tinge chini ya prodyuza Fresh boy.

"Nawaambia mashabiki wa muziki sasa nimeamka nipo kwenye mchakamchaka katika gemu, watarajie mambo mazuri, nahitaji sapoti yao kwani nimejipanga," amesema Jitu Baya.

Aidha amesema wimbo wa 'Kimewaka' upo mbioni kutengenezewa video kwa nguvu zake. Ameomba yupo tayari kuwa na menejimenti ya kusimamia kazi zake.



## INSTA-TWITTER



**Anayesafiri** kwa ndege anainjoi kufika haraka, anayepanda basi anainjoi kuona sehemu mbalimbali. Mwenye bando anainjoi ya mitandaoni, asiye na bando amepata uhuru wa kutokuwa teja wa mitandaoni. Maisha yana utajiri wa kutosha kumpa raha kila mmoja wetu, haijalishi ulipo na ulichonacho. Ni wewe tu na mtizamo wako-**Nikki wa Pilli.**



**Nikifa** nikazikwe Mbalizi, umeacha shilingi ngapi? Acha pesa basi-**Juma Lokole.**



**Sauti** ya kushoto inaniambia achana na muziki! Sauti ya kulia inaniambia ingia studio-**Ray C.**

Kuumbe!



AMKENI..AMKENI!

# Wastara, Z Anto wameanza tena

NI kitu gani kinachendelea kati ya mwanamuziki wa kizazi kipya, Z Anto na mwigizaji Wastara Juma?

Swali hilo bado lina utata kupata majibu, baada ya wasanii hao kuibua mjadala mkali katika mitandao ya kijamii kutokana kurushiana maneno makali, hasa kutoka kwa Wastara kuelekea kwa Z Anto.

Kibaya zaidi sakata hilo linawahusisha wake wa zamani wa mwanamuziki huyo ambao inadaiwa wanafanya harakati ya kurudi.

Hata hivyo, anayerushiwa mawe ni mpambaji wa video, Binti Kiziwi, ambaye inadaiwa siku za hivi karibuni amekuwa karibu na Z Anto, jambo ambalo linamuogopesha Wastara.

Z Anto ambaye ametambulisha singo yake mpya 'Nichape' alimshirikisha Binti Kiziwi kuipamba, lakini kitendo hicho kinaonekana kama ni hatari kwa Wastara.

Wastara ambaye inadaiwa mdogo wake kaolewa na Z Anto, ameamua kusimama kidete kulinda penzi la ndugu yake kwa kuanza kutoa onyo kali kwa mtu atakayeonekana kuwa adui.

Katika video zinazosambaa kwa kasi mitandaoni anaonekana Wastara akivalia bango suala hilo kwa kutoa tahadhari kwa Z Anto mwenyewe na Binti Kiziwi, kuwa makini vinginevyo wasijilaumu.

Anasema anawashangaa wanawake wanaolazimisha kuwa karibu na mwanamuziki huyo, wanatakiwa kuwa macho kwani wanaweza kupatwa na mabaya kama wasiporudi nyuma.

"Namshangaa Binti Kiziwi kujipendekeza kwa Z Anto, analazimisha ukaribu naye, namuonya akae mbali kwani anaweza kupata madhara makubwa," amesikika akisema Wastara.

Bila ya kufafanua kwa undani uhusiano wao, Wastara ameeleza kwamba wanawake wote wanajitokeza hivi sasa walimkimbia baada ya kuona amefulia kimuziki.

"Nawashangaa sana baada ya kuona sisi tumemnyanyua na kumuweka hapa alipo, wameanza kuleta maneno na kujipitisha... Ole wao," akaongeza.

Akizungumzia mtafaruku uliopo kati ya wanawake hao, Z Anto, amesema kwa upande wake hapati shida kwani yeye ni mwanaume shababi ni lazima apendwe.

"Mimi jabali ni mwanaume kamili kabisa, sichagui kupendwa na mwanamke wa aina gani, kwangu mke ni mwanamke wa kipekee sana," amesema bila kusema amemlenga nani.





NYOSHI

SONYO

HAMZA KALALA

# Bendi zilizochanua na kunyauka

Na Adam Fungamwango

MWISHONI mwa miaka ya '90 na mwanzoni mwa mwaka 2000, kulizuka mapinduzi makubwa ya muziki wa dansi.

Bendi hizo kwa asilimia kubwa zilikuwa zikipiga muziki kwa kuiga bendi za Wenge na Extra, lakini baadaye baadhi ya wanamuziki wakawa wabunifu, wakizitafsiri kwa kiswahili, au kutunga mashairi kwa lugha ya kiswahili.

Hapo ndizo tulipoziona bendi zilizokuja kuwa maarufu kama Diamond Musica maarufu kama Wana Dar es Salaam Kibindankoi, FM Academia, African Stars 'Twanga Pepeta', TOT Plus Band, African Revolution 'Tamtam' na nyingine nyingi.

Hizi ni bendi zilizotingisha hasa nchi, zikiwa na wanamuziki wengi walioondokea kuwa maarufu kama Allan Mulumba Kashama, Adolf Mbinga, Ramadhani Masanja 'Banza Stone', Ali Choki, Mwinjuma Muumini na wengine wengi.

Waswahili wanasema kuwa kwenye msafara wa mamba na kenge wamo. Kwa bahati mbaya sana kipindi hicho kuliundwa baadhi ya bendi zilizoondokea kuwa tishio kwa bendi maarufu kama Diamond Sound, Twanga Pepeta, lakini zikavuma kwa muda mfupi tu kabla hazijafa vifo vya ajabu.

Na zilipokuwa zikivunjika, baadhi ya wanamuziki wao vinara walikuwa wakichukuliwa na bendi kubwa.

**MCHINGA SOUND**

Ni bendi iliyoanzishwa na mheshimiwa Mudhihir M Mudhihir, wakati huo akishika nyadhifa mbalimbali za Uwaziri serikalini. Ikumbukwe kuwa mheshimiwa huyo pia ni mtunzi mzuri hasa kwenye muziki wa taarab na muziki pia. Kwenye taarabu aliwatungia TOT wimbo wa "Kijeba', na kwenye bendi yake aliyoianzisha alitunga kibao cha 'Mti wa Mpingo'.

Ndiyo iliyowaibua kina Muumini. Ilipoanzishwa ilitishia ustawi wa bendi za Twanga Pepeta na Chumvi Chumvi ambayo baadaye ikageuka kuwa Tamtam, hata FM Academia.

Hata hivyo haikudumu, ikafa na kuwaachia mashabiki wengi wa muziki simanzi kutokana na vibao vyao vikali ilivyotoa.

**STONO MUSICA**

Bendi hii imetoka kwenye ubavu wa FM Academia. Ni baadhi ya baadhi ya wanamuziki wa bendi hiyo ambao wengi ni raia wa Congo DR, kukamatwa na kuishi nchini bila kibali. Walipotoka walirejea FM Academia, lakini baada ya kutoa albamu moja tu ya 'Prisons' iliyotokea kuwa tishio, baadhi walijiengua na kwenda kuunda bendi ya Stono Musica chini ya Ndanda Kosovo wakajiita 'Wajelajela Original', yaani wao ndiyo hasa wale waliofungwa jela na si waliobaki FM Academia.

Iliishi kwa muda mfupi tu na kutoa vibao vikali kama 'Chini ya Ulinzi' 'Chocolate' na 'Binadanu'.

**BETA MUSICA**

Iliundwa na baadhi ya wanamuziki kutoka bendi mbalimbali zizokuwa na wanamuziki wengi wa Kikongomani kama FM Academia, Stono Musica, na Diamond Sound. Beta ilidumu kwa kipindi kifupi sana na wimbo wake maarufu sana ni 'Bana Beta'.

**CHUCHU SOUND**

Ni moja ya bendi matata sana, iliyosumbua bendi nyingi jijini Dar na Tanzania nzima. Yenyewe ilikuja na mageuzi makubwa, kwani pamoja na kupiga muziki wa aina ya bendi zingine, lakini ikaongeza na mduara ndani ikiwa na kina Jenico Flower, Omari Mkali, King Jiovani na wengineo.

Haijulikani ni nini kilisababisha bendi hii iliyopendwa mno ivunjike kwa muda mfupi tu, ikiwa ina vibao vikali kama 'Marafiki', 'Sitishiki', 'Hodi Hodi' na nyinginezo.

**MOKIBO SOUND**

Bendi hii ilianzishwa Mabibo jijini Dar es Salaam, nayo ni moja kati ya bendi zilizoanzishwa na kuleta ushindani mkubwa kwenye muziki wa dansi, lakini zikafa kifo cha ghafla na wanamuziki wake kusambaratika.

IMETOKEA

# Wanaume wapelekwa kuishi katika nchi sio yao

SEREN Idaho anasema hajawahi kwenda Sierra Leone wala kuishi nchini humo hadi alipohamishiwa huko kutoka Marekani miezi sita iliyopita.

"Sina ninayemfahamu hapa," analalamika Idaho ambaye ni baba wa watoto wawili.

Akionekana mgonjwa na mwenye kutaabika hata anapotembea, aliketi kwenye kiti cha plastiki kwenye chumba cha hoteli moja katika mji wa Freetown.

Alikuwa anazungumza huku akivuta sigara na kuangusha vipande vya vishungi ndani ya kifaa kilichopo pembeni yake.

Anasema kwamba afadhali hapo kulikuwa kuzuri kuliko gerezani ambapo alilala sakafuni huku akipambana na mende, panya na kunguni kwa miezi mitano.

Prince Latoya, 47, alikuwa kwenye ndege hiyo hiyo iliyokuwa ikiwaondoa katika hali hiyo hiyo.

Wanaume wote wawili ambao hawakuwahi kujuana hapo kabla , walikuwa ni wakazi wa kudumu Marekani. Lakini anasema kwamba wao wanatoka Caribbean, ila mamlaka husika iliwakana.

Idaho na Latoya pamoja na raia 17 wa Sierra Leonean na wengine wa Afrika Magharibi walikuwa wamehukumiwa kwa kufanya uhalifu nchini Marekani.

Waliishia kuingizwa kwenye ndege na kuwarejesha nyumbani baada ya ubalozi wa Sierra Leone mjini Washington DC kupata shinikizo kutoka kwa maofisa wa Marekani kulingana na Isha Sillah, mkuu wa maeneo ya Marekani na Pasifiki katika wizara ya nje.

Anasema kwamba mamlaka ya Uhamiaji Marekani iliwasilisha nyaraka katika ubalozi na kusemekana kwamba wanaume hao wawili ni raia wa Sierra Leone. Bila ya nyaraka zao kupitiwa , maofisa wa ubalozini waliwapa vyeti vya dharura vya kusafiria.

Ubalozi ulisema kwamba kile kilichofanya wao kuchukua hatua kama hiyo, ilikuwa ni shinikizo kutoka kwa Idara ya Uhamiaji na mambo ya ndani ya kuwakubali kama raia wa Sierra Leone..

Wizara ya mambo ya nje imewasiliana na balozi za nchi mbili za Caribbean mjini Washington kuthibitisha kwamba wanaume hao wawili ni raia wa nchi hizo.

"Ubalozi wa Dominican umekanusha kwamba Idaho ni raia wake huku ubalozi wa Bahamia ukisema kuwa nyaraka zaidi zinahitajika ili iweze kufanya uamuzi, ''amesema Bi. Sillah.

Lakini hadi kufikia sasa wamekwama katika hotelini.

Maneja, Osman Kamara, alisema kwamba wawili hao walitafutiwa hoteli hiyo na polisi lakini gharama ya kulipia chumba hicho ikawa ya juu na nusura wafukuzwe.

Kabla ya hapo kila mmoja wao alikuwa anapokea dola 2.50 kugharamia mahitaji yao ya kila siku lakini walisema ziliweza kununua kiamsha kinywa na chupa ya maji ya kunywa pekee.






DENTI

# Ugomvi wa wazazi, wanaoumia watoto

**Na Adam Fungamwango**

WAGOMBANAPO mafahari wawili ziumiazo ni nyasi. Huu ni msemo wa Kiswahili wenye maana kubwa yenye kutahadharisha kwamba inapotokea tatizo kwa watu wenye uwezo, basi wanaoathirika ni wale wa chini.

Mtunzi wa filamu ya 'Denti' amejaribu kuliangalia hili ndani ya jamii na kuja na kitu kama hiki kwa ajili ya kuelimisha.

Mara nyingi wanapogombana wazazi, wao hawaathiriki sana na ugomvi huo kwa sababu kila mmoja ana mtazamo wake au malengo yale, lakini watoto ambao wanawategemea baba na mama kuwa kitu kimoja, kukaa pamoja na kuwalea ndiyo wanaoteseka na athari za zao huonekana mapema zaidi kuliko hata za wanaogombana wenyewe.

Waliocheza filamu hii ni Blandina Chagula aliyecheza kama mke wa Deo, Slim Omari ambaye ndiye Deo mwenyewe, Gladyness Steve aliyecheza kama Linda, Ofisa Omari Thageo Alexander na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa Deo na mkewe wakigombana kiasi cha kupigana. Binti yao Linda anashuhudia ndondi hizo, lakini anaonekana kuumizwa mno na tabia ya wazazi wake ambao kila kukicha wao ni kubishana, ugomvi na ngumi. Mawazo kichwani wanamfanya hadi kutofanya vema darasani. Walimu wanashangaa kwani awali alikuwa denti mwenye akili nyingi.

Linda analieleza tatizo la wazazi wake kwa rafiki yake wa jirani. Hakuna rafiki mwema, kwani anamshauri kujisahaulisha mambo hayo kwa kunywa pombe, na anasa. Anakataa kufanya hivyo. Lakini kila kukicha ni afadhali ya jana. Mwisho anaamua kuungana na rafiki yake. Linda anabadilika tabia. Anaanza kunywa pombe, kufuta sigara na kufanya ngono zembe.

Siku moja mama yake anaondoka na kurudi usiku wa manane na kuomba afunguliwe mlango. Mumewe Deo anakataa na kumwambia akalale huko huko alikotoka. Anampiga marufuku Linda kwenda kumfungulia mama yake.

Hali inazidi kumchanganya Linda, ikawa ni tabia yake akitoka shuleni anapitia kwa wanaume zake kwa ajili tu ya kuondoa msongo wa mawazo kwa sababu ya matatizo ya nyumbani kwao.

Siku moja anaamua kwenda anakokutana na rafiki zake, lakini hawakuti. Anajaribu kwenda kijiwe kingine anakutana na mvulana anayemtongoza ili kufanya naye mapenzi. Akakubali, lakini wakati wanaingia chumbani tu, anakutana na wavulana wengine wawili ambao wote wanambaka.

Hali hiyo inazidi kumchanganya Linda na anaamua kutokwenda kabisa shule. Kama kawaida wazazi wa Linda wanaanza kugombana kutokana na kubadilika kwa tabia ya binti yao kila mmoja akimtuhumu mwenzake.

Walimu wake wanaamua kumsaka kwa sababu hafiki shule na nyumbani hakai sana. Wanamfuma kwa mpenzi wake akiwa hajiwezi kwa kutumia madaya ya kulevya.

Walimu anamchukua na kumpeleka hospitalini ili apate matibabu. Wanawasiliana na wazazi wake, lakini wanapokutana hospitalini kazi ni ile ile tu, ugomvi.

Walimu wanawaamua na kuwakalisha chini wakiwaambia kuwa ili kuokoa maisha ya mtoto wao, asiendelee na tabia aliyonayo, ni wao kuyamaliza yote na kuishi kwa amani nyumbani, vinginevyo wanampoteza mtoto wao. Wakaahidi kubadilika tabia mbele ya walimu wa binti yao.

WAMETISHA

# Prince Harry, Meghan hivi ndivyo wataishi



NI Picha zinazotoa mwanga wa namna Mwanamfalme wa Uingereza, Harry na mkewe Meghan Markle, watakavyokuwa baada ya kuanza maisha mapya nje ya ufalme.

Katika picha ambazo zimeibua gumzo katika mitandao ya kijamii, inawaonesha wanandoa hao wakijifunika mwamvuli wakati mvua ikinyesha.

Meghan na Harry walifanya iwe rahisi kwa mapaparazi kupata picha nzuri katika tukio hilo ambalo Harry na Meghan walionekana kama mastaa wakubwa wa sinema.

Muda wote Prince Harry na Meghan walikuwa wakitabasamu wakati wakihudhuria sherehe za utoaji tuzo huko Uingereza.

Wenzi hao ilikuwa mara yao ya kwanza kuhudhuria tuzo ya Mfuko wa Endeavor huko London siku Alhamisi, wiki iliyopita.

Wakati wakielekea ukumbini, mvua kubwa ilinyesha na ndipo walipoamua kujifunika kwa mwamvuli wakati walipokuwa wakitembea.

Lilionekana tukio la kushangaza kutoka nyuma ya wanandoa hao.

Wanawafalme hao kuonekana kama Sussex ni alama ya kwanza ya kumaliza majukumu kadhaa ya kifalme yatakayokoma siku zijazo wanapomaliza kazi yao ya mwisho.

Itakumbukwa kuwa, Prince Harry na mkewe, Markle walishtua ulimwengu wakati walipotangaza kwamba watajiondoa katika shughuli za kifalme na kuwa watu wa kawaida.

Wanandoa hao walitangaza habari hiyo ya kushtua kupitia ukurasa wao rasmi wa Instagram Januari 8, 2019.

Kuna taarifa kwamba Prince Harry na mkewe, Meghan Markle wote wamepigwa marufuku kutumia lebo ya 'Sussex Royal' baada ya tangazo hilo.

Wanandoa hao walioana mwaka 2018 kwenye harusi iliyohudhuriwa na nyota kibao.




# Katy hongera kuitwa mama kijacho

MKALI wa muziki wa Marekani, Katy Perry na mpenzi wake Orlando Bloom, wanataraji kupata mtoto wao wa kwanza.

Mwimbaji huyo wa kibao 'Never Worn White' ameonekana akiwa amevaa gauni kubwa linalovaliwa na wajawazito.

Orlando Bloom na Katy Perry walichumbiana mwaka 2019 na ujio wa mtoto huyo utakuwa Baraka kwa wawili hao.



## Pole Lanre yote mipango ya Mungu

MWIMBAJI wa Injili kutoka Nigeria, Lanre Teriba, maarufu kama Atorise, amekimbizwa hospitali baada ya kushambuliwa na watu wenye silaha.

Taarifa zinaeleza tukio hilo limetokea siku ya Jumamosi iliyopita, nje ya jiji la Lagos wakati msanii huyo alipokuwa akirejea nyumbani baada ya kumaliza kuburudisha katika sherehe ya harusi.

Alisema imekuwa ni maajabu ya Mungu kwa yeye kuendelea kuishi kutokana na tukio lilivyotokea na hakuamini kama atapata nafuu alipokimbizwa hospitalini.

## Juliet wamekusoma ushauri wako

MWIGIZAJI nyota kutoka Nollywood, Juliet Njemanze, amesema katika uhusiano, mapenzi huanza kwanza kabla ya kufikiria pesa.

Juliet amesema kuondoka ni chaguo lake la kwanza kama suala la mapenzi halitokuwapo.

Kulingana na mahojiano yake, mrembo huyo amesema hata angepatia pesa zote duniani. Hawezi kuwa na furaha endapo mapenzi yanakuwa hayamtoshelezi.





## Maskini Weinstein, kumbe si mzima

IMEELEZWA kwamba mtayarishaji maarufu wa filamu wa Marekani, Harvey Weinstein, hawezi kutumikia kifungo cha muda mrefu gerezani kutokana na kudhoofika kiafya.

Wakili wa Weinstein, ameiambia mahakama kwamba asipewe adhabu inayoweza kumsababishia maafa kiafya. Mchezaji huyo wa zamani wa sinema anakabiliwa na kifungo cha miaka mitano baada ya kukutwa na hatia ya makosa ya kuwanyanyasa wanawake kijinsia.

"Hali halisi ya Weinstein haiwezi kumudu mazingira magumu ya muda mrefu." Alisema wakili huyo.

## Kofi Olomide wavuruge tena Wakenya uone

MWANAMUZIKI wa Congo DRC, Koffi Olomide, hatimaye atapanda jukwaani nchini Kenya kutoa burudani baada ya kufukuzwa miaka minne iliyopita kufuatia tukio la kumshambulia mnenguaji wake.

Kulingana na Gazeti la National, mwimbaji huyo wa kibao cha 'Selfie' alizuiwa kuingia nchini humo na Idara ya Uhamiaji kutokana na kadhia hiyo, lakini sasa ameruhusiwa kutoa burudani baada ya kuomba radhi mashabiki wake.

Olomide anatarajia kwenda nchini humo akitoka Tanzania ambako alitoa burudani ya kibabe na kuwapagawisha mashabiki wake.



SAFU



## MIONZI YA SHERIA

Na John Juma
0716217615

# Mzazi aliyetengana na mkewe alazimishwi kiwango cha matunzo ya mtoto

BAADHI ya taarifa za msingi kuhusu jinsi mfumo wa sheria za familia zinafanya kazi kuhusu mipango ya uzazi wakati watu wanapoachana. Hazitolewi ushauri wa kisheria. Kama unafikiria kuachana au umeshaachana, unatakiwa kuomba ushauri wa kisheria kabla ya kufanya uamuzi kuhusu kitu cha kufanya.

Kutengana na watoto

Wakati unapotengana, mpenzi wako wa zamani atahitaji kufanya uamuzi muhimu kuhusu malezi ya watoto.

Sheria ya Familia ya 1975 ni sheria inayoonyesha kitu kinachotokea kwa familia zilizoachana kuhusu kutengana, mipango ya malezi, mali na utashi wa matengenezo.

Sheria inasema ni muhimu kwa watoto kuwa uhusiano mzuri na kila mzazi na watu wengine ambao ni muhimu katika maisha yao (kama mababu na mabibi), kama ni kwa ajili ya faida ya watoto na labda kama inawaweka watoto katika hasara ya kuumizwa.

Sheria inalazimisha wazazi kufanya juhudi za kutatua matatizo ya ulezi bila kwenda mahakamani. Wazazi wanatakiwa kufikia makubaliano kuhusu mipangilio ya watoto wao na jinsi ya kupata huduma ya kutatua matatizo ya kifamilia, kama vile upatanishi, ili kuwasaidia kufikia makubaliano.

Unyanyasaji wa majumbani katika uhusiano unaweza kuathiri jinsi sheria inavyofanya kazi. Ni muhimu kujulisha mwanasheria wako kama unahangaika, au umepatwa na vurugu za majumbani.

Kufanya mpangilio baada ya kuachana

Baada ya kuachana, ni muhimu kuangalia mpangilio wa kuishi wa watoto wako, ikijumuisha kiasi cha mda utakaotumiwa, na jinsi mtakavyowasiliana, ninyi kama wazazi. Ni muhimu kuangalia jinsi maamuzi ya mbeleni yatakavyotatuliwa kuhusu watoto.

**Usuluhishi ni mchakato ambapo wewe na mpenzi wako wa zamani mnaweza kujadili mipango kwa ajili ya watoto wenu. Hufanyika katika uwepo wa mtu anayejitegemea na asiyependelea aitwaye 'mpatanishi'. Mpatanishi hawezi kukushauri au kufanya uamuzi kwa ajili yenu, Kazi yao ni kuwasaidia wazazi kufikia makubaliano, kwa pamoja.**

Unaweza kuzungumza na mwanasheria ili kupata ushauri na msaada kuhusu mipangilio mnayoweza kuifanya. Wewe na mpenzi wako wa zamani mnaweza pia kuhudhuria suluhisho la mizozo ya familia kama vile upatanisho.

Suluhisho la mizozo ya familia na upatanishi

Usuluhishi ni mchakato ambapo wewe na mpenzi wako wa zamani mnaweza kujadili mipango kwa ajili ya watoto wenu. Hufanyika katika uwepo wa mtu anayejitegemea na asiyependelea aitwaye 'mpatanishi'. Mpatanishi hawezi kukushauri au kufanya uamuzi kwa ajili yenu, Kazi yao ni kuwasaidia wazazi kufikia makubaliano, kwa pamoja.

Wakati mkifikia makubaliano ambayo wote wawili mnayafurahia, yanaweza kuwa kumbukumbu kama 'mpango wa uzazi' au 'ridhaa ya maagizo'. Unapaswa kupata ushauri wa kisheria kabla ya kusaini mpango wa uzazi au maagizo ya ridhaa.

### Ridhaa ya Maagizo

Ridhaa ya Maagizo ni mkataba ulioandikwa ambao hupitishwa na Mahakama. Una nguvu kisheria sawa na amri inayotolewa baada ya kesi kusikilizwa Mahakamani. Wewe na mpenzi wako wa zamani mnaweza kuomba ridhaa ya maagizo bila ya kwenda Mahakamani.

### Kwenda mahakani

Kama makubaliano hayawezi kufikiwa, unaweza kuuliza Mahakama kuamua kuhusu mipango yenu ya uzazi

Kabla ya kwenda Mahakamani, wewe na mpenzi wako wa zamani mnatakiwa kuhudhuria suluhisho la mizozo ya famila, kama vile upatanishi.

Uhitaji huu wakati mwingine unaweza kuondolewa ikiwa kuna wasiwasi unaohusiana na vurugu za familia au unyanyasaji wa watoto.



## KALAMU YA MWALIMU

Na Reubeni Lumbagala
0764-666349.

# Hofu, kutojiamini adui wa wanawake

JUMA lililopita katika Safu hii ya Kalamu ya Mwalimu ilichapishwa makala iliyokuwa na kichwa cha habari; Mkombozi wa mwanamke ni yeye mwenyewe. Makala hiyo ilikuwa maalum kwa wanawake na ilikuwa miongoni mwa makala zilizoandikwa na waandishi mbalimbali katika Siku ya Wanawake Duniani inayoadhimishwa kila ifikapo Machi 8, kila mwaka.

Kutokana na unyeti wa Siku ya Wanawake Duniani, mjadala wa masuala ya wanawake nimeupa uzito kuuendeleza juma hili ili kutoa mchango wangu wa mawazo kwa wanawake wa Tanzania.

Katika makala ya juma lililopita, nilielezea namna mwanamke alivyokuwa mdau mkubwa kufanikisha masuala mbalimbali ya kimaendeleo kwani mchango wao unahitajika kutokana na uwezo wao wa kifikra na utambuzi.

Pia nilisisitiza namna ambavyo wanawake wanavyopaswa kupambana wenyewe ili kufikia usawa wa kijinsia na kisha kunufaika na fursa mbalimbali zinazomzunguka.

Kiujumla, makala iliweka mkazo mkubwa katika kuwafumbua macho wanawake wapambane wenyewe, waache kukaa, kusubiri huruma na msaada wa wanaume ili kuweza kufikia mipango na ndoto mbalimbali walizonazo.

Adui mkubwa wa wanawake katika kufikia malengo yao ni hofu na kutokujiamini. Katika kufikia mafanikio ya aina yeyote, uthubutu na kujiamini ni nguzo muhimu kwani pasipo haya, ni vigumu kupiga hatua.

Kutokana na uwezo mkubwa ambao wanawake wameuonesha katika kusimamia majukumu mbalimbali waliyonayo kuanzia ngazi ya familia hadi Taifa, hakuna shaka kuwa wanaweza kufanya mambo makubwa yatakayokidhi matarajio ya jamii.

Tatizo la uwepo wa mila na desturi potofu na mfumodume katika jamii, kumewajengea wanawake hofu na kutokujiamini kupitiliza.

Hofu na kutokujiamini kumewaponza na kuwafanya wabaki nyuma hata katika masuala yanayowagusa wao wenyewe na hivyo wakati mwingine kubaki wakisubiri msukumo kutoka kwa wengine.

Ili kushinda vita hiyo kunahitajika dhamira ya dhati isiyoyumbishwa na mwingine yeyote. Narudia tena, ni muhimu kuwa na dhamira ya dhati isiyoyumbishwa na mwingine ili kushinda hofu na kutokujiamini.

Wanawake wakiwa bado wapo katika tafakuri ya siku yao duniani, ni muhimu kuzingatia kuwa siku wakatayomshinda adui hofu na kutokujiamini, hakutakuwa na yeyote wa kuweza kuzuia mafanikio yao.

Upo umuhimu mkubwa kwa wasichana na wanawake kusoma kwa bidii kwani elimu ni mkombozi wa fikra. Fikra za wanawake zitakapokombolewakupitia elimu, kujiamini kutajengeka na hivyo kuwa na uthubutu katika masuala mbalimbali kama kufanya biashara, kufungua kampuni na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Mwanamke aliyeelimka vyema, anajiamini vya kutoshana hatakubali kusikiliza maneno ya kukatisha tamaa ambayo ni adui wa mafanikio.Mwanamke lazima awe anaamini kuwa yeye ni tofauti kiuumbaji , lakini linapokuja suala la uwezo, uthubutu, ana uwezo sawa na hata zaidi ya mwanamume.

Wanawake waishi kwenye ndoto zao, wakiamini kuwa wao wenyewe wanawajibu wa kuzitimiza ndoto, maono na malengo yao.

Kama mtu ataamua kumsaidia mwanamke katika harakati zake za kimaendeleo, liwe jambo la ziada lakini wasisubiri mwingine aje kumsaidia huku akijidanganya kwa ile msemo 'Mwanamke akiwezeshwa anaweza'. Mwanamke anayesubiri kuwezeshwa hakika ndoto zake zitachelewa kutimia au zitashindikana kabisa. Hii itakuwa hasara kwake.

Uwepo wa wanawake wengi waliofanikiwa katika elimu, biashara na uongozi iwe ni shamba-darasa kwa wanawake wengine kujifunza kwa wenzao.

Mazingira na changamoto za wasichana na wanawake wa Tanzania yanafanana kwa sehemu kubwa, hivyo wasikubali kutoa visingizio vya kushindwa kutimiza malengo yao. Mwanamke ajiulize, aliyefanikiwa ana nini kikubwa cha ziada?

Ujasiri na kujiamini ni nyenzo ya kushinda changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake katika jamii. Hakuna wa kumsaidia katika kupambana na vita ya hofu na kutokujiamini, bali ni mwanamke mwenyewe kuamua kuingia ulingoni kupambana hadi tone la mwisho. Ni kheri kushindwa katika ulingo wa mapambano, kuliko kubaki nyuma kuogopa mapambano.

Hata pale itakapotokea akadharauliwa katika maono yake, aamini kuwa maono yale ni yake mwenyewe, na wa kuyatimiza ni yeye mwenyewe. Kuomba msaada wa mawazo kutoka kwa wengine ni jambo jema na linasaidia kupata mawazo mbadala, lakini wanawake wasitarajie mara zote watapata mawazo chanya. Ifahamike kuwa si mwanamke tu, bali hata mwanamme; atakayeshinda vita ya hofu na kutokujiamini, hakika atafanikiwa. Wanawake changamkeni zaidi, nafasi bado ipo, hamjachelewa.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.

***Maoni: (+255) 764 666349.***

# WANAWAKE WALETA MAPINDUZI TPA



Baadhi ya wafanyakazi wanawake wa Mamlaka ya Bandari (TPA) wakitoa msaada Hospitali ya Taifa ya Muhimbili jijini Dar es Salaam.

**Na Elizabeth Zaya**

MACHI 8 mwaka huu wanawake kote duniani waliadhimisha 'Siku ya Mwanamke Duniani' kwa kufanya shughuli mbalimbali ikiwamo makongamano na kusaidia jamii.

Baadhi ya shughuli nyingine ambazo wanawake hao huzifanya katika siku hii ni pamoja na kutembelea na kutoa misaada kwa makundi yenye uhitaji na kufanya usafi katika maeneo mbalimbali.

Katika baadhi ya mashirika na taasisi mbalimbali, huwaachia wanawake kuendesha shughuli za uzalishaji mali kama kitendo cha kuunga mkono uwezo wao.

Kauli mbiu ya siku ya wanawake duniani mwaka huu ilikuwa ikisema 'Kizazi chenye usawa kwa maendeleo ya sasa na ya baadaye'.

Miongoni mwa walioitendea haki kauli mbiu hiyo ni wanawake wanaofanya kazi katika Mamlaka ya Bandari Tanzania(TPA), ambao kabla ya kilele cha siku hiyo walifanya shughuli mbalimbali za kijamii.

Miongoni mwa shughuli ambazo wanawake hao walifanya ni pamoja na kufanya usafi katika maeneo mbalimbali ya fukwe za bahari ya Hindi.

Pia walikwenda kuwatembelea watoto wanaoishi katika vituo vya kulelea watoto yatima vilivyopo Kigamboni na Tandale jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake wa TPA, Leticia Mutaki, anasema wanawake wana uwezo mkubwa wa kufanya kazi, kulea na hata kusaidia jamii.

"Mwanamke ana umuhimu mkubwa katika jamii, yeye ni mama na mlezi wa familia, ni kioo cha jamii na pia mfanyakazi na mchangiaji mzuri wa pato la taifa kupitia shughuli mbalimbali za kimaendeleo.,"anasema Mutaki na kuongeza "Zamani wanawake walikuwa wanaonekana kama si chochote kuanzia kwenye ngazi ya familia hadi maofisini, lakini kwa sasa wanakuja kwa kasi, wanajishughulisha sana, hakuna mwanamke anayekaa bila kitu cha kufanya siku hizi, hata wale ambao hawajaajiriwa, wamejiajiri wenyewe kupitia ujasiliamali."

Anasema katika siku za hivi karibuni, wanawake wamekuwa pia wakisimama na kufanya vizuri katika nafasi mbalimbali za uongozi tofauti na ilivyokuwa katika miaka ya nyuma.

"Kwa sasa tunao wanawake kwenye taasisi mbalimbali za serikali na binafsi ambao ni wakurugenzi na wanaongoza vizuri sana, na wengine tunawashuhudia wanasimama kwenye majukwaa ya kisiasa ni Mawaziri, wabunge, madiwani, wanafanya vizuri na na wana ujasiri mkubwa,"anasema Mutaki.

Mutaki anasema miaka ya nyuma wanawake ndani ya TPA, walikuwa hawapewi nafasi ya ajira wakihofiwa kwamba kazi zinazofanywa katika mamlaka hiyo ni ngumu ambazo hawawezi kuzimudu, lakini kwa sasa mambo yamebadilika.

Anasema kwa sasa wanapata ajira na wanafanya kazi kama ilivyo kwa wanaume na wakati mwingine kuwazidi kabisa hasa ukizingatia kwamba hivi sasa bandari zimeboreshwa na zinatumia vifaa.

"Zamani watu waliokuwa wakifanya kazi TPA ni wanaume tu, wanawake walikuwa hawapewi nafasi ya ajira kwa sababu walisema kazi zinazofanywa hapo ni ngumu na za kubeba mizigo, hivyo hawaziwezi, lakini sasa hivi mambo yamebadilika wanawake wanafanya kazi vizuri na ukizingatia kwa sasa tunatumia vifaa vya kisasa kubebea mizigo tofauti na ilivyokuwa zamani,"anasema Mutaki.

Anaongeza: "Wanawake wa TPA sisi katika ufanyaji kazi wetu hatulilii asilimia 50 \50 tunapambana na wanaume bega kwa bega na tunaamini siku za usoni wanaume wao ndiyo watakakuwa wanailila hiyo maana tutakuwa tumewapita mbali."

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Deusdedit Kakoko, anasema wanawake wamekuwa na mchango mkubwa katika shughuli za uzalishaji pamoja na matokeo mazuri ya ukusanyaji wa mapato yanayoonekana katika mamlaka hiyo kwa sasa.

"Sisi TPA tunawathamini sana wanawake, ni kundi ambalo ukiwa nalo kazini unakuwa na uhakika wa kufanya vizuri kwa sababu hulka yao ni kufanya kazi kwa bidii na pia ni waaminifu kwa kila jambo wanalokuwa wanafanya,"anasema Kakoko .

Aidha akasisitiza kwa kusema "Kwa sasa tunafanya vizuri sana kuboresha bandari zetu na hata mapato yetu yamepanda kwa kiwango kikubwa tofauti na miaka ya nyuma kidogo, nataka nikiri kabisa hapa kwamba miongoni mwa watu wanaochangia mafanikio yote haya ya TPA ni pamoja na kundi hili muhimu la wanawake."

Katika hafla hiyo, Mutaki aliiomba serikali kuzingatia kutoa haki stahiki kwa wafanyakazi wa mamlaka hiyo ikiwamo kupandishwa madaraja, kuwa na utaratibu wa kutoa bonasi kwa wanaofanya kazi vizuri zaidi pamoja na maboresho ya mishahara.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika ambaye anakiri kwamba kwa sasa wanawake wanafanya kazi kubwa na nzuri katika nafasi mbalimbali wanazoshikilia.

Pia anasema kwamba uwapo wa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan katika nafasi hiyo kumechangia kuleta hamasa kwa wanawake wengi kuingia katika nafasi za uongozi .

Anasema Tanzania imefanya mageuzi makubwa katika kuwapatia nafasi wanawake na kuwaomba kujitokeza kwa wingi katika uchaguzi mkuu mwaka huu kuwania nafasi mbalimbali za kisiasa.

"Uwapo wa Makamu wa Rais wa kwanza mwanamke, kumeleta hamasa kubwa kwa wanawake kuingia katika nafasi mbalimbali za uongozi," anasema Mkuchika

Mkuchika anaeleza kwamba kutambua uwezo mkubwa walionao wanawake katika kuleta mabadiliko katika jamii, ipo haja ya kuendelea kuwathamini, kuwalinda na kuwaendeleza.

Anasema takwimu za ulinganifu katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita inaonyesha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika kutoa nafasi za uongozi kwa wanawake.

mwisho

MAKALA



Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa LHRC, Hellen Kijo-Bisimba (kushoto), akitoa ushauri wake kwenye uzindizi wa mtandao huo. Katikati ni Mkurugenzi wa Women Find Tanzania, Mary Rusimbi na Mkurugenzi Mtendaji wa KIWOHDE, Justa Mwaituka.

# MBINU ZAANIKWA UTETEZI HAKI ZA BINADAMU

**Na Sabato Kasika**

WANAWAKE Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (WHRD), unaoshirikisha mashirika yasiyo ya kiserikali zaidi ya 50, wamezindua rasmi mtandao wao jijini Dar es Salaam.

Uzinduzi huo ulifanyika Jumatano ya wiki hii na kuhudhuriwa wadau mbalimbali wa kutetea haki za binadamu, wakiwamo wakongwe katika Nyanja hiyo ambao ni Hellen Kijo-Bisimba, Justa Mwaituka na Mary Rusimbi.

Kijo-Bisimba alikuwa wa kwanza kuelezea uzoefu wake katika kazi ya utetezi wa haki za binadamu, na kuwakumbusha watetezi hao kwamba wasitegemee kupata kipato kutokana na kazi hiyo kwa kuwa ni ya kujitolea.

Katika kuelezea uzoefu wake kwenye masuala ya kutetea haki za binadamu, Kijo-Bisimba anasema, watetezi hao wanapaswa kukumbuka kuwa kazi hiyo inataka moyo na uvumilivu.



Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Vickness Mayao (katikati), akikata utepe kama ishara ya kuzindua rasmi mtandao huo **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

Kutokana na ukweli huo, anawataka waanzilishi wa mtandao huo kufanya kazi kwa moyo wote bila kutanguliza maslahi mbele, kwani vinginevyo wanaweza kujikuta wasifikie malengo.

"Kama kati yenu kuna mtu anadhani kuwa utetezi ni ajira, ni bora atafute kazi nyingine ya kufanya, kwani hii ni ya wito, wakati wowote unafuatwa na watu kusikiliza matatizo yao," anasema Kijo -Bisimba.

Anasema, katika utetezi wa haki za binadamu, maslahi kuwa ni kwa yule anayetetewa na siyo mtetezi atarajie kupata kitu kutoka kwa anayetetewa, na kwamba wanachama wa mtandao huo wakitambua hilo, watafika mbali.

"Huo ndiyo uzoefu wangu ambao nimeuona, katika miaka yangu yote ambayo nimedumu katika kazi ya kutetea haki za binadamu, kwamba hii siyo ajira bali ni kujitolea," anasema.

Kijo-Bisimba anawataka wadau wote kutimiza wajibu wao kikamilifu ili hatimaye lengo la kuhakikisha kunakuwapo na usawa ndani ya jamii na tena bila ukatili ukiwamo wa kijinsia linatimia.

Naye Mkurugenzi wa Women Fund Tanzania, Mary Rusimbi, anautaka mtandao huo kuhakikisha unasimama imara bila kuyumba kwa kuimarisha umoja na mshikamano.

"Majukwaa yanayotuunganisha ni muhimu sana, katika kuleta mabadiliko yenye tija kwa wote, na Women Fund Tanzania unaunga mkono, hivyo imarisheni umoja miongoni mwenu," anasema Rusimbi.

Rusimbi anasema, anatarajia kuona mtandao huo haugawi watu katika makundi na badala yake bila kujali umri, wawe wamoja na kuhakikisha lengo lao kutetea haki za binadamu linatimia.

"Nyie wote ni wamoja, endeleeni na umoja huo kwa kutambua kwamba umoja ni nguvu na mkiona taasisi imara, maana yake ni kwamba wahusika wana umoja, hivyo matarajio yangu ni kuona hilo katika mtandao huu," anasema.

Katika mchango wake wa uzoefu, Mwaituka anasema, kuna mambo kadhaa ambayo watetezi wa haki za wanawake na binadamu kwa ujumla wanatakiwa kuyazingatia ili waweze kufanikiwa.

"Kwanza kabisa ni kuwa na ajenda, kwani ukosefu wa ajenda ni kikwazo katika kutekeleza ajenda ya utetezi wa haki za binadamu nchini, hivyo jambo la kwanza ni kuwa na ajenda mnayoisimamia," anasema Mwaituka.

Anasema, utetezi wa haki za binadamu una changamoto zake ambazo ni muhimu kuzivumilia, vinginevyo wahusika wanaweza kufikia kukata tamaa badala ya kusonga mbele.

"Mnaweza kuitwa majina mengi ya kukatisha tamaa, lakini msirudi nyuma katika kazi hii kwani ina changamoto zake, na pia mjue mnachopambania, kiko eneo lipi kisheria au kikanuni, " anasema.

Mwaituka anasisitiza watetezi kutokuwa waoga wanapokutana na vikwazo mbele ya safari, kwa vile havikwepeki, bali kinachotakiwa ni kusimama imara hadi kuhakikisha wanafanikiwa.

"Kwetu sisi kwa miaka 20 wao KIWOHEDE tumepambania kutokomeza suala la changudoa bila kukata tamaa wala woga ingawa tulikumbana na changamoto nyingi, hivyo nanyi igeni mfano huu," anasema.

USHAURI

Kwa upande wake Ofisa Uchunguzi Mkuu wa Tume ya Haki za Binadamu, Philemon Thomas anazitaka taasisi zote zinazoshughulika na haki za binadamu, kuimarisha ushirikiano na serikali.

"Vilevile kazi zenu zisiwe Tanzania Bara tu bali na visiwani mjitokeze mfahamike ili muwahudumie hasa watu wa pembezoni, ambao mara nyingi wanakosa huduma za utetezi," anasema Thomas.

Thomas anautaka mtandao huo kufanya kazi kikamilifu na siyo kuishia njiani, lakini kikubwa zaidi anatarajia kuona ukiimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali ikiwamo serikali.

Naye mgeni rasmi katika uzinduzi wa mtandao huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto, Dk. John Jingu, serikali ina jukumu kubwa kwenye masuala ya wanawake kupitia mikataba mbalimbali ya kimataifa.

Kwa niaba yake, Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Vickness Mayao, anasema, uzinduzi huo ni hatua muhimu ya kutengeneza jukwaa litakaloangalia utekelezaji wa maeneo yote yaliyoanishwa Beijing.

"Cha msingi ni kwamba mtandao huu uzingatie vigezo vya usajili wake kwa usahihi ili iwe rahisi kufikia malengo, ambayo umejiwekea kwenye harakati za kutetea haki za wanawake na binadamu kwa ujumla wake," Mayao.

MAKALA

# AN NAHL WAWAFUNDA WANAFUNZI WANAOINGIA KIDATO CHA TANO 2020

**Na Moshi Lusonzo**

MAMBO yanayosababisha wanafunzi wanaojiunga na masomo ya juu kushindwa kufaulu vizuri ni pamoja na makundi, kutojitambua na kutojiamini.

Hayo yamebainika wakati wa kongamano la kuwapongeza wanafunzi zaidi ya 200 waliofanya vizuri kidato cha nne mwaka 2019 kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Kongamano hilo liliandaliwa na Taasisi ya An Nahl Trust kwa lengo kuwapongeza na kuwakutanisha wanafunzi hao kwa ajili ya kupata mbinu za kufanya vizuri wanapoingia kidato cha tano.

Akizungumza wakati akitoa mada, Profesa Fatma Manzi, kutoka Taasisi ya Utafiti ya Ifakara, amewataka wanafunzi kuona ngazi wanayoelekea ya kielimu ni kama wanaanza safari ya maisha yao.

Anasema kuna tatizo linalowasumbua wanafunzi kushindwa kufanya vizuri mara wanapojiunga na kidato cha tano, hali hiyo inatokana na kushindwa kwenda na mazingira husika, kuchagua makundi mabaya na kushindwa kujitambua.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa An Nahl, Mussa Mtasingwa, akizungumza na wanafunzi na wazazi katika kongamano la kuwapongeza

"Lazima mjitambue nyie ni nani na mnakwenda huko kufanya nini? Wengi wenu wanaona kama wamepiga hatua baada ya kufaulu na ndio maana wanajikuta wanafanya vibaya na hatimaye kushindwa kutimiza ndoto zao," anasema Profesa Fatma.

Anasema kama mtoto atajitambua umuhimu wake katika jamii, lazima atasoma kwa jitihada kubwa ili aweze kuikomboa.

Amekemea vitendo vya kiharakati vinavyofanywa na baadhi ya wanafunzi pale wanapojiunga na elimu ya juu na kusababababisha kujiingiza katika mambo yasiyowahusu.

"Msiwe wanaharakati huko mnakokwenda, someni kwa malengo na kukumbuka nyuma kuna watu wanakuangalia na wanahitaji msaada wako," ameongeza kusema.

Anasisitiza kwamba kama kila kijana atawajibika na kutumia vizuri fursa ya elimu, ni wazi baadhi ya matukio machafu yatatoweka.

Sheikh Issa Othman Issa, anasema Mwenyezi Mungu amewaumba binadamu akiwahimiza kusoma na kujifunza mambo mapya kutoka kwa wengine.

Anasema ni jambo baya kama kijana atapenda mambo ya juu ambayo hana uwezo nayo, na kuacha kujifunza yale madogo ambayo yanaweza kumsaidia katika maisha yake.

"Kijana lazima ujue thamani yako na kuepuka mambo makubwa ambayo yanaweza kukuondolea utu na ubinadamu wakati ukitafuta elimu," anasema Sheih Issa.

Anaeleza kwamba Uislamu umewaongoza namna ya kuishi kwa kujua thamani na utu wa mtu, hivyo endapo vijana wakisoma elimu ya dini pamoja na ile ya kawaida wana nafasi kubwa ya kufaulu.

"Hakuna miujiza katika mafanikio ya mtu yoyote, lazima kuwepo na juhudi na uwepo wa Mungu ndipo kila kitu kitakwenda kama ulivyopanga," anasisitiza kiongozi huyo wa dini.

Awali Ofisa Mtendaji wa An Nahl. Mussa Nyamsingwa, amewataka wanafunzi hao kutokata tamaa na kujifunza mambo mapya kutokana na dunia ya sasa kuegemea teknolojia zaidi.

Amesema ni muhimu kujifunza mambo mapya kila siku na kuchagua makundi mazuri ya kujisomea ili kupata uwezo wa kimapokeo.

"Hakuna kitu kizuri kama kuchagua makundi mazuri ya kujisomea, hapo ndipo unaweza kupimwa kama uwezo wako wa kuamua na kufanya kazi kama unafanya kazi vizuri. Baadhi wanajikuta wakiingia katika mikono ya watu wasio salama na hatimaye anajikuta akipoteza muelekeo na hatimaye anafeli katika mithani yake," anasema Nyamsingwa.

Anasema vijana zaidi ya 200 waliopata bahati kushiriki kongamano hilo, ni muhimu wakatumia vizuri elimu wanayopatiwa na kwenda kufanya kwa vitendo pale watakapojiunga na kidato cha tano.

Mmoja wa wanafunzi aliyeongoza kwa kufanya vizuri mwaka jana, Abdulrahim Omar, ameipongeza Taasisi ya An Nahl kwa kuwakutanisha na amejifunza mengi kupitia kongamano hilo.

"Nimejifunza mambo mengi hapa, naahidi nitayafanyia kazi wakati napigania ndoto yangu ya kuwa daktari wa magonjwa ya saratani," anasema Omar.

Mwanafunzi huyo ambaye amemaliza shule ya sekondari ya Feza, amesema mafanikio aliyopata ni kutokana na kumtegemea Mungu kila anachokifanya pamoja na kusoma kwa bidii.

Amewashauri wanafunzi wenzake kujituma na kujifunzi wengine kwa juhudi kwa kila wanachofundishwa na walimu, huku wakiachana na mambo ambayo yanaweza kuwarudisha nyuma kitaaluma.

Baadhi ya wanafunzi waliofanya vizuri walikabidhiwa zawadi mbalimbali ikiwamo vitabu, vifaa vya kujifundishia na safari ya kwenda Umra.




Baadhi ya wanafunzi waliofanya vizuri katika mtihani wa kidato cha nne mwaka 2019 wakiwa na zawadi zao walizopewa na An Nahl

## HABARI KIMATAIFA

CORONA INAVYOITESA DUNIA

# Kenya, Ethiopia zathibitisha kuwa nao



Baadhi ya watu wakiwa wamevaa vitambaa puani wakiangalia miti ya maua katika mji wa Nanjing, mashariki mwa China. **PICHA: AFP**

MTU wa kwanza amethibitika kuwa na virusi vya corona nchini Kenya.

Waziri wa afya nchini humo, Mutahi Kagwe amethibitisha kisa hicho katika tangazo alilolitoa moja kwa moja kupitia vyombo vya habari.

Pia nchini Ethiopia mamlaka imetangaza kisa cha kwanza cha maambukizi ya corona. Mgonjwa wa Ethiopia ni raia wa Japan.

Mutahi amesema kwamba mtu mwenye maambikizi ya virusi vya Corona alithibitishwa kuwa ana maambukizi hayo Alhamisi usiku.

Waziri huyo amesema kwamba mgonjwa huyo amegundulika nchini Kenya tangu kuzuka kwa mlipuko huo mjini Wuhan nchini China.

Mgonjwa huyo ni raia wa Kenya aliyewasili nchini humo kutoka Marekani kupitia mjini London nchini Uingereza tarehe 5 mwezi Machi 2020.

Aligunduliwa kuwa na virusi hivyo katika maabara ya wizara ya afya nchini Kenya.

Hatahivyo waziri huyo amesema kwamba mgonjwa huyo ambaye ni mwanamke yuko katika hali njema na kwamba viwango vyake vya joto vimeshuka na kuwa vya kawaida.

"Tarahe 5 mwezi Machi aligunduliwa kuwa na virusi hivyo katika maabara ya serikali lakini sasa viwango vyake vya joto vimeshuka na kuwa vya kawaida anakula vizuri lakini hawezi kutolewa hadi virusi hivyo vitakapokwisha mwilini.", amesema Waziri Kagwe.

Waziri huyo amewataka Wakenya kuwa watulivu na kuacha wasiwasi. Amesema kwamba serikali ya Kenya kupitia wizara ya afya itaendelea kuimarisha mikakati ili kuhakikisha kwamba hakuna usambazaji wa virusi hivyo zaidi.

Kamati ya dharura ilioanzishwa ili kukabiliana na kuenea kwa virusi vya corona, itaendelea kutoa muongozo ili kukabiliana na ugonjwa huo hatari.

Wakatiu huo huo, mtu wa pili amepata maambukizi ya ugonjwa wa corona nchini Jamhuri ya kidemokrasi ya Congo.

Mtu huyo anadaiwa kuwa raia wa Cameroon aliyewasili nchini humo kutoka Ufaransa kulingana na mwandishi wa BBC mjini Kinshasa . Kwa sasa amelazwa hospitalini kwa matibabu. Wizara ya afya nchini humo imetoa wito kwa raia kuzingatia usafi wakati wowote.

Mgonjwa huyo ni raia wa umri wa miaka 46 ambaye anaishi DR Congo na familia yake .

Alirudi nchini humo kutoka Ufaransa mwezi Mei 8 na hakuonyesha dalili za virusi hivyo.

Mamlaka ya DR Congo inasema kwamba kufikia sasa imewatambua watu 117 waliogusana na wagonjwa wawili wa virusi hivyo.

### MKE WA WAZIRI MKUU CANADA APATA CORONA

Waziri Mkuu wa Canada, Justin Trudeau na mke wake watabaki kwenye karantini kwa siku 14, baada ya mkewe Sophie Gregoire Trudeau kukutwa na virusi vya corona.

> Shirika la Afya duniani limeutangaza mlipuko wa virusi vya corona kuwa ni janga la kimataifa, huku mlipuko huo ukiendelea kusambaa kwa kasi katika mataifa mbalimbali duniani.

Hata hivyo, imeelezwa Sophie anaendelea vizuri na dalili alizonazo si mbaya kwa mujibu wa mkurugenzi wa mawasiliano wa Waziri Mkuu.

Trudeau pia atakuwa kwenye karantini kama hatua ya tahadhari. Hatapimwa katika hatua za sasa kwa kuwa haoneshi dalili za maambukizi.

Katika ukurasa wa Twitter, Sophie aliandika "Nitarejea nikiwa na afya njema hivi karibuni,"

Siphie alisema alikuwa amepata dalili ambazo hazikuwa za kawaida na kuongeza kuwa kwenye karantini si kitu ukilinganisha na familia nyingine nchini Canada wanaopitia katika hali hiyo.

"Ninawatia moyo na kuwaweka kwenye fikra zangu,' nawatakia afya njema, alisema.

Rais wa Marekani Donald Trump amesema hana mpango wowote wa kupima virusi, ingawa alikaribiana na afisa kutoka Brazil ambaye sasa amegundulika kuathirika na virusi hivyo.

Ikulu ya Marekani imesema hakuwa na mazungumzo na ofisa huyo wa Brazil, hivyo hakukuwa na umuhimu wa kupima.

Fabio Wajngarten, Waziri wa mawasiliano wa rais wa Brazil Jair Bolsonaro, aliweka kwenye mtandao wa Instagram picha yake akiwa amesimama karibu na Rais Trump.

Rais wa Brazil Jair Bolsonaro, amechukuliwa vipimo na sasa anasubiri majibu.

Hatua hii imekuja baada ya mawasiliano aliyoyafanya na mkuu wake wa mawasiliano, ambaye amekutwa na virusi vya corona baada ya kurejea akitokea kwenye ziara nchini Marekani alipokutana na Rais Donald Trump.

Shirika la Afya duniani limeutangaza mlipuko wa virusi vya corona kuwa ni janga la kimataifa, huku mlipuko huo ukiendelea kusambaa kwa kasi katika mataifa mbalimbali duniani.

Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dkt Tedros Adhanom Ghebreyesus amesema kuwa idadi ya visa nje ya China vimeongezeka mara 13 kwa kipindi cha majuma mawili yaliyopita.

### UJERUMANI YAFUNGA SHULE, VITUO VYA WATOTO

Nchini Ujerumani baadhi ya majimbo yametangaza kuchukua hatua ya kukabiliana na virusi vya Corona kwa kufunga shule zote na vituo vya kulelea watoto.

Maofisa mjini Berlin wametangaza kuwa mji huo utaanza kuchukua hatua hiyo wiki ijayo. Pia wanafikiria kuzuia usafiri wa umma au kupunguza ratiba zake.

Hatua hizo zinachukuliwa katika kukabiliana na mlipuko wa virusi vya corona nchini Ujerumani.

Kituo cha televisheni cha n-tv nchini Ujerumani kimemnukuu meya wa Berlin, Michael Mueller, ambaye amesema shule zitakazoanza kufungwa Jumatatu ijayo ni zile za sekondari.

Wito umekuwa ukiongezeka nchini humo kuchukua hatua kali kama zile zilizochukuliwa na nchi jirani za Ulaya, kuzifunga shule ili kusaidia kupunguza kuenea kwa virusi vya corona.

Aidha, majimbo ya Saarland na Bavaria yametangaza hatua kama hiyo kuanzia Jumatatu . Jimbo la Bavaria limesema wanazifunga shule zote hadi mwishoni mwa likizo ya sikukuu ya Pasaka, katikati ya mwezi Aprili mwaka huu.

Aidha, majimbo mengine matatu ya Ujerumani likiwemo la North Rhine Westphalia jana yalitarajia kuamua kuhusu kuzifunga shule zake.

### WATU MAARUFU WALIVYOAMBUKIZWA CORONA

Watu maarufu wakiwamo wanasiasa, wanamichezo na waigizaji duniani ni miongoni mwa watu walioambukizwa na virusi vya corona.

Muigizaji nyota wa tuzo za Oscar Tom Hanks, na mke wake Rita Wilson wameambukizwa na maambukizi ya virusi vipya vya ugonjwa huo nchini Australia.

Hanks na mkewe Wilson, ambao wote wana miaka 63, walienda kupata ushauri wa daktari baada ya kuona wana dalili za mafua huko Queensland, kabla ya kuandika katika kurasa yake ya Instagram kuwa amepata virusi vya corona.

Huko Iran, makamu wa kwanza wa rais Eshaq Jahangiri, amegundulika ameathirika na virusi vya corona . Jahangiri ni kiongozi wa juu wa kisiasa ambaye amepata virusi hivyo ambavyo mpaka jana watu zaidi ya 354 wamefariki na 9,000 wameambukizwa.

Waziri wa afya na mbunge wa chama cha Conservative nchini Uingereza Nadine Dorries, amethibitisha amekutwa na maambukizi ya virusi hivyo.

Dorries, mbunge wa kwanza kugundulika na maambukizi hayo, alichukua tahadhari zote baada ya kubaini kuwa ameathirika.

# HADITHI


ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# MAUAJI HARUSINI-4

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**




**Na Adam Fungamwangwo**

WATOTO wa mjini wanamwita Kidaga. Sijui kwa nini. Lakini wazazi wake walimpa jina la Fadhili. Alizaliwa jijini Dar es Salaam. Alisomea na kukua kwenye jiji hilo. Kufahamiana na watu wengi tofauti wanjanja wanjanja wa mjini, kukimfanya kujiingiza kwenye kazi za kijanja, zilizowapatia pesa za haramu kwa muda mfupi.

Alishawahi kufanya kazi ya utapeli wa magari na nyumba na kumpatia pesa nyingi, alizojenga nyumba na kumfanya kuishi maisha ya fahari.

Pia, hakuwa mbali na ujambazi. Aliifanya kazi hiyo hasa alipoona kuwa ina fungu kubwa. Kutokana na kuwa ni mtoto wa Dar, alitumika kama ni mchora ramani, na ndiye aliyekuwa akipeleka habari kwa majambazi wenzake ni wapi kuna pesa, nani anapeleka pesa benki na lini. Dili inapofanyika yeye naye hupewa mgao wake.

Kazi nyingine kubwa na kusimamia kazi nzima na kuamrisha nini kifanyike wakati huo, au nini kisifanyike, lakini pia kujua njia, mitaa na maeneo mengi ya Dar es Salaam.

Kwenye operesheni hii alichukuliwa kama msimamizi mkuu. Yeye ndiye mratibu na wakati wa tukio atakuwa amebaki ndani ya gari lenye vioo vya giza akiwasiliana na Michael pamoja na Tamim ambao watakiwa nje wakikamilisha kazi ya kuhakikisha maharusi wanauwa.

Wakati huo, pia Kidaga atakuwa anawasiliana na bosi Abesh kuhusu nini kinaendelea sehemu ya tukio.

************************************

Tamim Hussein ndiyo jina lake. Alizaliwa mjini Iringa na kusomea huko. Alijiunga na Jeshi la Kujenga Taifa huko Mafinga.

Moja kati ya sifa zake kuwa ilikuwa ni kulenga shabaha. Makamanda walimpenda kutokana na kipaji chake kikubwa na kulenga shabaha. Walijua kabisa mbele ya safari atalisaidia Taifa kulinda nchi.

Pamoja na yote hayo, udhaifu waTamim ni kupenda starehe. Alipenda mno pombe na wanawake.

Akiwa kambini, siku moja aliwashawishi wenzake wananne na yeye watano kutoroka na kwenda mjini kuponda raha. Walikwenda na kurudi. Ilikuwa ni Mwenyezi Mungu tu aliyewalinda, kwani kambi ilipo ilikuwa ni katikati ya pori ambalo lina wanyama wakali hasa chui.

Lakini kutokana na ukame wao wa kukaa miezi mitatu kambini bila pombe wala wanawake, waliamua liwalo na liwe. Walipokuwa kwenye kumbi moja Iringa mjini, licha ya kufanya starehe zao kwa kunywa pombe, lakini walipora wanawake wa watu na wanaume zao walipotaka kuzuia uhalifu huo waiishia kupigwa.

Ilikuwa ni kama majaribio baada ya mazoezi ya miezi mitatu. Alitaka kuonyesha kuwa wameiva kijeshi.

Waliwatwanga jamaa, wakachukua wanawake zao. Usiku ile ule walipomaliza haja zao waliondoka kuwahi kambini kabla hakujakucha.

Na kweli walifanikiwa bila kuuawa na wanyama wakali. Hata hivyo duniani hakuna siri. Habari zilitapataa kuwa kuna wanaume watano walipigwa na kunyang'anywa wanawake zao kwenye ukumbi wa starehe.

Katika uchunguzi wao, polisi kwa kushirikiana na jopo la madaktari walithibitisha kuwa waliowapiga raia hao, hawakuwa watu wa kawaida. Huenda walikuwa ni watu waliokuwa na mafunzo maalum.

Ndipo minong'ono ilipozuka kuwa walikuwa na wanajeshi wa JKT Mafunga waliotoroka kambini.

Habari zikamfikia mkuu wa kambi ambayo kwa kushirikiana na polisi waliamua kufanya gwaride la utambulisho baada ya majeruhi kupona.

Kwa asilimia 100, majeruhi waliwatambua watesi wao, mmoja wapo akiwa ni Tamim.

Mkuu wa kambi alisikitishwa mno na kitendo kile. Hakutegemea mwanafunzi wake aliyemtegemea Tamim kufanya kitu kama kile.

Mkuu hawakusikitishwa na vijana wake wanne, ila Tamim kwa sababu alikuwa na kipaji maalum. Kipaji cha kulenga shabaha. Na alijua kuwa taifa lilikuwa linaelekea kupata mtu.

Hata hivyo ni lazima sheria ifuate mkondo wake. Wakafukuzwa jeshi wote watano na kukabidhiwa kwa Jeshi la Polisi kwa ajili ya kuwafungulia mashtaka na kuwapeka mahakamani.

Mwisho wa siku wote walifungwa jela miezi sita kwa kosa la kujeruhi. Alipotoka Tamim alirejea nyumbani kwao Iringa. Hata hivyo mazingira sasa ya maisha kwake yalikuwa magumu. Awali alitegemea kuwa akimaliza jeshi apate kazi.

Lakini kwa sasa hakuwa na uhakika wa kupata kazi yoyote. Akaamua kwenda jiji la Dar es Salaam kusaka ajira yoyote ile ambayo inaweza kumfanya asogeze siku.

**Lakini kwa sasa hakuwa na uhakika wa kupata kazi yoyote. Akaamua kwenda jiji la Dar es Salaam kusaka ajira yoyote ile ambayo inaweza kumfanya asogeze siku.**

Aliingia kwenye mikono ya vijana wajanja wa mjini, walioweza kufanya kazi yoyote ile halali na haramu, ili mradi tu wapate pesa.

Akaingia kwenye kazi ya utapeli. Ikampatia pesa. Siku isiyo na jina akiwa kijiweni kwake Ilala Bungoni alifika mtu mmoja wa makamu hivi. Alipokelewa na mmoja kati ya marafiki zake. Wakaenda pembeni na kuteta.

Rafiki yake hiyo, Seif, alirudi kwa wenzake na kuwapa mchongo kuwa jamaa alikuwa anahitaji mtu wa kazi na kama kuna mtu anamfahamu, basi ampeleke.

"Kazi gani." Aliuliza Tamim.

"Kazi ngumu, siyo kama hii tunayoifanya. Jamaa anatafuta mtu anayeweza kumuua mtu aliyemdhulumu mali zake." Seif alisema na kuwatazama wenzake waliokuwa kwenye benchi kijiweni hapo.

"Jamaa kadhulumiwa mzigo, sasa jamaa kila anapofuatilia anamzingua, halafu kwa siku za karibuni akaanza kumtishia maisha. Sasa kaona bora yeye amuwahi kabisa. Kama kuna mtu anamfahamu anayeweza kuifanya kazi hiyo ampeleke na yeye atapata cha juu."

"Mwambie aje tuelewane, hiyo kazi mimi naweza kuifanya." Tamim alijibu kwa kujiamini na kusababisha mshangao na mshtuko kwa pamoja kwa wenzake.

Wanachojua ni kwamba Tamim na wao ni matapeli, wanaopata pesa kwa kudanganya watu na si kukaba, au kuua, inakuwaje leo mwenzao aonyeshe kuwa anaweza kazi hiyo, ili mradi tu anayetaka kufanyiwa kazi hiyo awe na bastola?

Ni shilingi milioni mbili tu ndizo zilizomuingiza Tamim kwenye dili hilo, huku rafiki yake Seif alilamba shilingi laki mbili kwa ajili ya kuendesha bodaboda tu. Alichotaka ni kupewa picha ya anayehitajika kufa, lakini pia mawasiliano kuwa yuko wapi.

Siku ya tukio, simu ilipigwa na kuambiwa kuwa yupo kwenye gari aina ya noah, ilitoka Ilala kwenda Buguruni.

Kwa sababu wao wenyewe walikuwa Ilala hawakuna na papara. Walikaa tayari na wakaliaona gari hilo likipita. Wakalianganisha kwa nyuma, Seif akiendesha na Tamim kuwa nyuma kama abiria hivi. Hakuna yoyote aliyekuwa akijua nini kinaendelea zaidi yao tu.

Seif aliambiwa aendeshe bodaboda hadi awe pembeni ya gari lile. Gari lilipokuwa sambamba na pikipiki, Tamim aliona ndani ya gari kulikuwa na watu watano pamoja na dereva, hivyo ilikuwa ni vigumu kujua mlengwa ni yupi pamoja na kuwa ana picha yake. Alichofanya akaita jina lililopo kwenye picha ya mlengwa 'Ally?" Aliita.

Mwenye jina hilo alitoa kichwa dirishani. Alikuwa katikati ya siti ya nyuma. "Wapite kwa kasi." Tamim alimwambia Seif. Waliokuwa kwenye gari walishangaa mtu kumwita mwenzao, lakini hakumwambia kitu. Hata hivyo na wao walipotezea.

Bodaboda lilikata mtaa mmoja kuiruhusu gari ipite. Seif na Tamim walirejea tena kwenye barabara kuu baada ya gari kupita. Ilikuwa kama kona ya Barabara ya Mandela na Uhuru, ameneo ya Buguruni Mataa. Mita kama hamsini hivi, Tamim alichomoa bastola na kulenga kwenye kioo cha nyuma sehemu ya katikati, akaachia risasi mbili zilizotoboa kioo na kuzusha taharuki eneo hilo. "Geuza Bodaboda turudi." Alimwambia Seif. Saa chake baadaye habari zikaja kuwa Ally amefariki baada ya kupigwa risasi na watu wasiojulikana.

Kazi hiyo ilimpa heshima kubwa kwa wahalifu, hasa shabaha yake. Akapata tenda zaidi na zaidi. Hivyo ndivyo alivyoingia kwenye kazi hiyo na kupata tenda ya kuua maharusi Grace na Patiyo.

ITAENDELEA JUMAMOSI

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

mu: +255 26 2324455
ax: +255 26 2323233
arua Pepe: ps@mow.go.tz
vuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 13/03/2019

### TANGAZO

. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAPILI tarehe 15/03/2020 kampuni ya **CIVIL LOTHS ENTERPRISES LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa. Kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **SONGEA** gari hilo lina namba za usajili:

**T392 DPZ/ T 295 DGR**

. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 17.80 |
| Upana | - | mita | 3.0 |
| Kimo | - | mita | 4.60 |

. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM hadi SONGEA kupitia LINDI**

xxxxxx

Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**unaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**


NIPASHE NI JIBU LAKO


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI NA. 121/2013**

**MUCHUNGUZI B. KAIJAGE........................MDAI**
DHIDI YA
1. GODIAN RICHARD .......................................................
2. KELEPIN EDWARD KAMUGISHA...................................
3. MELANIA ALCHARD ................................... WADAIWA

**KWA MUCHUNGUZI B. KAIJAGE**
**(POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa madai Na. 121/2013 yamepangwa kutajwa tarehe 16/03/2020 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 16/12/2020

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

115668002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI**
**MAHAKAMA YA MWANZO..MAKOLE**
**WILAYA YA DODOMA**
**MADAI NAMBARI 12/2020**
**MDAI....COSTANSIA NELSON**
**DHIDI YA**

**MDAIWA..GODWIN ZAKARIA –MFANYA BIASHARA ARUSHA- 0768552018**
**KWA GODWIN ZAKARIA**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai **YA TALAKA KUACHANA**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe 23/03/2020 saa 08:00 asubuhi kwa kujibu madai hayo kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hakuhudhiria siku ilitajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha umepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa. Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 13/03/2020.

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo

115668502

### PASIPOTI IMEPOTEA



**GODWIN CHRISTOPHER MATHEW** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba AB 864906. iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam mwaka 2017.

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.**

**Taarifa ya polisi:**
**DAR/CEN/RB/227552Z/2020.**

156682

### KUPOTEA KWA VYETI



**Arizina Mussa** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cha kidato cha nne chenye ***index namba P0222/0025*** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2005 katika shule ya Sekondari Zanaki, cheti kingine cha kidato cha nne chenye **index namba P1072-0013** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2005 Katika shule ya Sekondari Kamene ..

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**DAR/TAB/RB/226397/2020**

15668302

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BEATRICE PAUL NG'WANASAYI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 985 DFV TOYOTA PASSO. Chassis namba KGC100183944. Engine namba KGC100.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MBD/RB/572/2020.**

115668402


Uza, Chenye Thamani Kubwa

Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa

Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SOLSKJAER: POGBA ATABAKIA MAN UTD 2020-21



**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amebainisha kwamba, anatarajia Paul Pogba kuwapo Manchester United msimu ujao.

Pogba amecheza mechi saba tu za Ligi Kuu msimu huu, kutokana na kuumia enka tangu Desemba mwaka jana.

Hata hivyo, kukosekana kwa kiungo huyo hakujaiathiri klabu hiyo kwa wiki za hivi karibuni, huku United ikifikisha mechi 11 bila kufungwa kwenye mashindano yote na walipata ushindi wa 5-0 dhidi ya LASK kwenye mchezo wa Ligi ya Europa hatua ya 16, Alhamisi.

Licha ya Pogba kuendelea kuwa majeruhi na kutoeleweka kwa majaliwa yake ya baadaye, Solskjaer amesema kwamba nyota huyo wa Ufaransa atabaki kama mchezaji wa United.

Na baada ya kushinda dhidi ya LASK, kocha wa 'Mashetani Wekundu' hao alikwenda mbele zaidi, akisisitiza mchezaji huyo wa zamani wa Juventus bado atakuwa hapo kwenye dimba la Old Trafford msimu wa 2020-21.

"Paul ni mchezaji wetu. Ana miaka miwili imebaki kwenye mkataba wake, pamoja na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja zaidi," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Unaweza kumtarajia Paul kuwa hapa, hilo halina shaka kabisa nina uhakika ataendelea kuwa mchezaji wa Man United msimu ujao."

# Corona yaahirisha mechi kufuzu Kombe la Dunia

**SAO PAULO,** Brazil

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa (Fifa), limethibitisha kwamba mechi za mwezi huu za Mataifa ya Amerika Kusini za kufuzu Kombe la Dunia 2022, zimeahirishwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Shirikisho la Soka la Amerika Kusini, CONMEBOL, liliomba kuahirishwa kwa mechi za kufuzu kwa ukanda huo, zikiwamo mechi kati ya Brazil vs Bolivia na Argentina vs Ecuador kutokana na mlipuko huo, ambao umegharimu karibu maisha zaidi ya watu 5,000 duniani kote.

Katika taarifa iliyotolewa Alhamisi, Fifa ilionyesha kwamba, bado haijapanga mechi hizo mbili zitachezwa lini, ambapo awali zilipangwa kuchezwa kati ya Machi 23 na 31, mwaka huu.

"Fifa itaendelea kuangalia hali jinsi ilivyo na itaamua lini mabadiliko hayo yatafanyika," ilisema taarifa yake.

CONMEBOL pia ilithibitisha kuahirishwa kwa muda michuano ya Kombe la Klabu Bingwa Amerika Kusini, Libertadores, kutokana na mlipuko wa ugonjwa huo.





# *Pereira nje msimu mzima Euro 2020*

**LONDON,** England

BEKI wa Leicester City, Ricardo Pereira, atakosa kipindi chote cha msimu kilichobaki na pia kuna uwezekano wa kuikosa michuano ya Mataifa ya Ulaya, Euro 2020, baada ya kuumia mguu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno aliumia kwenye goti wakati Leicester ikiibuka na ushindi wa 4-0 dhidi ya Aston Villa kwenye mchezo wa Ligi Kuu, Jumatatu.

Kocha Brendan Rodgers amethibitisha kwamba beki huyo wa kulia hatakuwepo kwenye kikosi hicho kwa msimu wote uliobaki.

"Hatutakuwa na Ricardo Pereira kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki. Aliumia goti," alisema Rodgers Alhamisi.

"Hajafanyiwa operesheni. Yupo na timu ya madaktari. Ni pigo kubwa kwetu. Ni nafasi kwa mwingine.

"Tutaangalia namna mambo yatakavyokuwa na mchezaji mwenyewe hali yake itakavyokuwa. Hatujajua atakaa kwa kipindi cha miezi mingapi nje ya dimba."

## HABARI MICHEZO

# CORONA KUPEPERUSHA DENMARK VS ENGLAND



**COPENHAGEN,** Denmark

SHIRIKISHO la Soka la Denmark (DBU), linatarajia mchezo kati ya timu yake ya taifa dhidi ya England uliokuwa ufanyike Machi 31, mwaka huu utafutwa kutokana na hofu ya kusambaa kwa virusi vya ugonjwa wa corona kwenye nchi za Scandinavia.

Jumatatu wiki hii, Waziri Mkuu wa Denmark, Mette Frederiksen alitangaza matukio yote ya mkusanyiko wa watu kuahirishwa kwa wiki mbili, huku pia DBU ikisimamisha michezo yote ya Ligi Kuu ya nyumbani hadi Machi 29, mwaka huu.

Denmark ilipanga kucheza mchezo wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya Visiwa vya Faroe mjini Herning Machi 27 kabla ya kwenda kwenye dimba la Wembley siku nne baadaye kucheza na England.

Katika taarifa ya DBU, ilieleza wamejiandaa kuahirishwa mechi zote hizo kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya Corona.

Mkurugenzi wa DBU, Kenneth Reeh alisema: "Denmark inahuzuni katika hali hii, ambayo imeathiri soka la Denmark.

"Kama ilivyo kwa jamii nyingine yoyote, tunalichukua tukio hil kwa umakini mkubwa na bila shaka yoyote, tunasitisha matukio yote ya mikusanyiko ya watu pamoja na mechi za soka, hadi wiki chache zijazo."

England bado ratiba yake inaonyesha watacheza mchezo wa kirafiki na Italia kwenye Uwanja wa Wembley Machi 27, mwaka huu.

# Ferdinand amjia juu Mourinho

**LONDON,** England

BEKI wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand, amesema Jose Mourinho ndiye chanzo cha Tottenham Hotspur kutupwa nje ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Tottenham ambayo msimu uliopita ilicheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuchapwa na Liverpool, msimu huu ikiwa chini ya Mourinho imeyaaga mashindano hayo ikiwa hatua ya 16-bora.

Spurs ambayo kwa sasa kwenye msimamo wa Ligi Kuu England ipo nafasi ya nane, ilichapwa nje ndani na RB Leipzig ya Ujerumani na kutupwa nje ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa jumla ya mabao 4-0.

Ikiwa nyumbani Uwanja wa Tottenham jijini London ilichapwa bao 1-0 kisha Jumanne usiku ikaangushiwa kipigo cha 3-0.

Na Ferdinand sasa anaona Mourinho hakutimiza moja ya majukumu yake ya kuwaweka tayari kiakili na kisaikolojia wachezaji wake.

"Hakuwaandaa wachezaji wake kisaikolojia," alisema Ferdinand akinukuliwa na gazeti la Daily Mail.

Akaongeza kwamba, kama kocha hakutimiza majukumu yake, hivyo lawama zote za kutolewa kwa Spurs yeye ndiye mhusika."



# Rais Barcelona bado ana nia na Neymar



**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, hajakataa au kukubali juu ya uwezekano wa kumsajili tena Neymar kutoka kule Paris Saint Germain.


Ingawa Bartomeu alithibitisha kuwa wakati wa majira ya joto yaliyopita walijaribu mara mbili kumrudisha Neymar Nou Camp, bila mafanikio kwa sababu klabu yake iligoma kumuuza, licha ya kupokea ofa hizo mbili za Barcelona.

Bosi huyo wa Barcelona amedai kuwa licha ya Neymar kuiburuza timu hiyo mahakamani akidai baadhi ya malipo yake ya nyuma, hilo halitahusika katika kufanya uamuzi wa mwisho wa kuamua kama wamsajili au la.

Wakati akidai kuwa lolote linaweza kutokea kwenye ishu ya usajili wa Neymar, kuhusu Philippe Coutinho, ambaye yuko Bayern Munich kwa mkopo, amedai hajui nini kitaamuliwa mwisho wa msimu iwapo auzwe au abakizwe.

Neymar licha ya kuwa na rekodi nzuri tangu alipotua katika klabu hiyo ya mji mkuu wa Ufaransa mwaka 2017, hajawa na msimu mzuri mara hii kutokana na kusumbuliwa na majeraha kwa muda mrefu.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA, HUDSON-ODOI WAPATA CORONAVIRUS

## Wachezaji Arsenal kujitenga, mechi dhidi ya Brighton yaahirishwa huku...

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta, amejitenga na kikosi hicho baada ya kubainika kuwa na virus chanya vya corona, huku pia winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi akiwa mchezaji wa kwanza kutoka Ligi Kuu England kubainika kukumbwa na virusi hivyo, 'coronavirus'.

**Mechi ya Arsenal dhidi ya Brighton iliyokuwa ichezwe leo, Jumamosi sasa imeahirishwa lakini hadi jana asubuhi kulikuwa bado hakujatolewa uamuzi rasmi wa kuhusu kuahirishwa kwa mchezo wa leo kati ya Aston Villa na Chelsea.**

Uongozi wa Premier League ulitarajiwa kufanya "mkutano wa dharura na klabu" jana kujadili mustakabali wa baadaye wa ratiba ya ligi hiyo.

Chelsea imeeleza Hudson-Odoi "alionyesha dalili zinazofanana na baridi kali Jumatatu asubuhi" na kukaa mbali na uwanja wa mazoezi.

Klabu hiyo iliongeza kuwa mchezaji huyo "anaendelea vizuri na anatarajia kurejea uwanja wa mazoezi haraka kadri iwezekanavyo".

Kwa upande wa Arsenal 'The Gunners', ilifunga uwanja wao wa mazoezi na viongozi ambao hivi karibuni waligusana na Arteta pia watapaswa kujitenga.

"Ukweli hili linakatisha tamaa," alisema Mhispania Arteta, 37. "Nilifanya vipimo baada ya kujisikia vibaya. Nitarejea kazini mapema nitakaporuhusiwa."

Arsenal imesema inatarajia "idadi kubwa ya watu" watajitenga, ikiwamo "kikosi kizima cha kwanza".

Klabu hiyo ilitakiwa kuvaana na Brighton kwenye mechi ya Ligi Kuu katika Uwanja wa Amex leo, lakini Brighton, ilitoa taarifa kwa ufupi baada ya kuthibitishwa Arteta amepatwa na maambizi ya virusi vya corona, ikitangaza kuwa mchezo huo hautafanyika.

Mkurugenzi Mkuu wa Brighhton, Paul Barber alisema: "Kwanza kabisa mawazo yetu yapo na Mikel Arteta na tunamtakia kupona haraka.

"Ni muhimu kabisa kwa afya na ustawi wa watu binafsi inachukua kipaumbele na kwa kuzingatia kwamba mechi ya Jumamosi imeahirishwa.

"Tunaomba radhi kwa mashabiki wote kwa usumbufu utakaojitokeza, lakini amini kila mmoja ataelewa kuwa tunakabiliwa na hali isiyokuwa ya kawaida.

"Uongozi wa Premier League umetangaza kuwa jioni hii [juzi] kwamba utafanya mkutano wa dharura na viongozi wa klabu zote kesho asubuhi [jana], na tutaendelea kuwafahamisha ratiba itakavyotolewa lini na wakati tutakapokuwa katika nafasi ya kufanya hivyo."

BBC Sport ilieleza kutambua kuwa klabu zote 20 za Ligi Kuu zinataka kuamua juu ya mkakati wa pamoja, na chaguzi mojawapo ambayo wangeijadili katika mkutano huo ni kuahirisha mechi zote za wikiendi hii.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL YAMTAKA PARTEY

ARSENAL inajiandaa kutoa ofa majira ya joto kwa kiungo wa Atletico Madrid, Thomas Partey. Mghana huyo mwenye umri wa miaka 26, ana kipengele kinachomruhusu kuuvunja mkataba wake kwa pauni milioni 45. ***(Telegraph)***

### JUVE, ARSENAL KWA WILLIAN

JUVENTUS itatoa ushindani kwa Arsenal na Tottenham katika mbio za kumsajili Willian ambaye atakuwa huru msimu huu, Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 30, atamaliza mkataba wake na Chelsea majira haya ya joto na inaelezwa anapendelea kuendelea kubaki London. ***(Tuttosport via Sport Witness)***

### NEVILLE KUJIUZULU ENGLAND

PHIL Neville anafikiria kujiuzulu kuinoa timu ya Taifa ya Wanawake ya England baada ya kuchezea kichapo kwenye mechi nane kati ya 12. ***(Mail)***

### CORONA KUIKAWIZA ARSENAL

ARSENAL inatarajia mechi zao mbili zitaahirishwa baada ya Kocha Mkuu, Mikel Arteta kupatwa na virusi vya corona. ***(Mirror)***

### KLABU KUWAZUIA WACHEZAJI

KLABU za Ligi Kuu England hazitaki kuwaruhusu wachezaji kwenda mapumziko wakati wa kupisha ratiba ya mechi za kimataifa baadaye mwezi huu kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona. ***(Mail)***

### UEFA KUAHIRISHA EURO 2020

UEFA na Vyama vya Klabu za Ulaya vitapendekeza kuahirishwa kwa michuano ya Euro 2020 kwa mwaka mmoja ili kutoa nafasi kwa ligi za Ulaya kuchelewa kutokana na coronavirus. ***(Mirror)***

### EVERTON YAMTEGA BELOTTI

EVERTON inavutiwa kumsajili mshambuliaji wa Italia, Andrea Belotti, kutoka Torino. ***(Calciomercato- in Italian)***

### IGHALO KUFUNGWA JUMLA UTD

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema amefungua milango ya kumsajili jumla Odion Ighalo anayeichezea klabu hiyo kwa mkopo. Straika huyo wa Nigeria mwenye umri wa miaka 30, amefunga mabao manne katika mechi nane alizocheza tangu alipojiunga na na klabu hiyo akitokea Shanghai Shenhua Januari mwaka huu. ***(Manchester Evening News)***

### ZIYECH AMTAKA ONANA

MSHAMBULIAJI ajaye Chelsea, Hakim Ziyech, 26, anatumai kuiwezesha klabu hiyo kumsajili kipa Mnigeria Andre Onana, 23, kutoka klabu yake ya sasa, Ajax. ***(Mail)***

### EPL ZAMTIMUWA SANCHO

BORUSSIA Dortmund ipo tayari kumruhusu Jadon Sancho kuondoka majira ya joto yajayo kama ataomba kuondoka. Winga huyo wa England mwenye umri wa miaka 19, anatakiwa na Liverpool, Manchester United na Chelsea. ***(Standard)***

### VITESSE YAMTAKA GALLAGHER

VITESSE Arnhem inavutiwa kumsajili kiungo wa Chelsea na England U-21, Conor Gallagher, 20, kwa mkopo katika msimu ujao. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

## KMKM yajigamba kutetea ubingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa timu ya KMKM inayocheza Ligi Kuu ya Zanzibar, Ame Msimu, amesema bado ana matumaini makubwa ya kuutetea ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana visiwani hapa, kocha huyo alisema tangu anauanza msimu huu malengo yake yalikuwa kuutetea ubingwa wake kwa mara nyingine licha ya kutambua kuwa jitihada zaidi zinapaswa kufanywa na wachezaji kwa kujituma uwanjani.

Alisema kikosi chake kipo vizuri na hakuna mchezaji majeruhi, hivyo hali hiyo inampa matumaini makubwa ya timu hiyo kufanya vizuri hadi mwisho mwa msimu na kunyakuwa ubingwa wa Zanzibar.

Aidha, akizungumzia mchezo wake wa kesho dhidi ya timu ya Mwenge yenye makazi yake Kisiwani Pemba, alisema wamejiandaa kushinda ili kupata alama tatu zitakazoendelea kuiweka timu hiyo katika nafasi nzuri zaidi.

"Mchezo wetu wa Jumamosi [leo], nimejiandaa kupata alama tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri zaidi katika msimamo wa Ligi Kuu, kwa jinsi ligi inavyoelekea, kupoteza mchezo ni kupoteza nafasi ya kufanya vizuri," alisema

KMKM ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 43, huku Mwenge wakiwa nafasi ya 14 na alama zao 13 katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

## Tegere aahidi kuipaisha Azam

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Azam FC, Nevere Tegere, amesema ana matumaini ya kufanya vizuri na kusaidia timu yake kupata matokeo mazuri kutokana na kujituma kwake na kuonyesha juhudi anapokuwa mazoezini na katika mechi.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, nyota huyo alisema ana imani na uwezo wake wa kufumania nyavu na atapambana kutumia vizuri kila anapopewa nafasi ya kucheza ili kuhakikisha wanafikia malengo yao.

Alisema sababu inayomfanya awe anafanya vizuri na kutupia mabao, mazoezini mara kwa mara ni pamoja na mazoezi anayoyafanya akiwa peke yake baada ya kumaliza program ya timu.

"Nimekuwa nikifanya mazoezi nikiwa uwanjani pamoja na wachezaji wenzangu pia nikiwa mwenyewe ninafanya mazoezi ya binafsi ya kufunga jambo linaloniongezea uwezo wa kufunga kwenye mechi," alisema Tegere.

Alisema mipango yake ni kuhakikisha anaonyesha juhudi na kujituma pale anapoamini na kupewa nafasi ya kucheza katika kikosi kinachoanza kila mechi.

"Kwa muda mfupi niliocheza soka Tanzania, nimeona changamoto zake ikiwa ni pamoja na ugumu wa ligi, hivyo nina imani nitapambana na changamoto hizo kuonyesha kile ambacho kinatarajiwa kutoka kwangu," alisema.

Tegere amejiunga na Azam kwenye usajili wa dirisha dogo akitokea klabu ya FC Platinum ya Zimbabwe na tayari ametupia jumla ya mabao matatu kwenye mechi zake mbili mfululizo alizocheza.

# SHIME AAHIDI TANZANIA KUISHANGAZA UGANDA LEO

**Na Somoe Ng'itu,** KAMPALA

WAKATI timu ya soka ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17, ikitarajiwa kuwavaa wenyeji Uganda katika mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KCCA Lugogo jijini hapa, Kocha Mkuu wa kikosi hicho cha Tanzania, Bakari Shime amesema "tumekuja kupambania matokeo chanya".

**Kikosi cha Tanzania kitashuka uwanjani kikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-1 walioupata katika mchezo wa kwanza uliochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam wiki mbili zilizopita.**

Mshindi wa jumla katika mechi ya leo, atakutana na mshindi kati ya Ghana au Liberia ambayo ilikubali kichapo cha mabao 2-0 katika mchezo wa kwanza uliochezeshwa nchini kwao.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa jana, Shime alisema wamekuja kupambana na watahakikisha wanakamilisha malengo yao ya kuondoka na ushindi katika mchezo huo.

Shime alisema mechi itakuwa ngumu kwa pande zote mbili, lakini atataka kuona kikosi chake kinapata bao la mapema ili kujilinda zaidi na kujipunguzia presha.

"Tumekuja kwenye mapambano, tunajua nusu ya kazi tuliifanya nyumbani na huku tumekuja ugenini kumalizia, hatutajilinda tu, tutahitaji pia kushambulia ili kuongeza mtaji wa mabao," alisema Shime.

Amewataka wachezaji wake kutobweteka na matokeo ya ushindi waliyopata katika mechi tatu za nyuma walizocheza, badala yake kujituma zaidi ili kukamilisha mtihani unaowakabili wa kufuzu kucheza fainali hizo za dunia kwa mara ya kwanza.

Naye Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Oscar Mirambo, alisema anatarajia kuona mechi ikiwa ngumu, lakini hawawadharau wapinzani wao licha ya kuwa mbele kwa matokeo.

"Tunaingia uwanjani tukiwa na faida ya kuwa mbele, lakini hii haitoshi, benchi la ufundi limejipanga kuhakikisha katika mechi ya kesho (leo), tunashinda pia, wachezaji wote ni wazima na hili linatufanya tuzidi kumshukuru Mungu, tunaomba pia tuamke salama kesho (leo), ili kukamilisha mipango yetu," alisema Mirambo.

Tanzania ilisonga mbele katika mashindano hayo baada ya kuifunga Burundi jumla ya mabao 6-1 wakati Uganda yenyewe iliwaondoa Ethiopia kwa kuwachapa 5-1.

TUNAWEZA...



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko jijini Dar es Salaam, wakiwa kwenye mazoezi ya mpira wa kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kocha KMC afunguka walipoishika Yanga*

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwashika 'pabaya', Yanga katika mechi ya Ligi Kuu Bara kwa kuwapa kipigo cha bao 1-0 kwenye Uwanja Uhuru jijini Dar es Salaam juzi, Kocha Msaidizi wa KMC FC, Habibu Kondo ametoa siri ya ushindi huo.

Licha ya kutoka kuifunga Simba kwa bao 1-0 Machi 8, mwaka huu, juzi Yanga ilishindwa kufurukuta mbele ya KMC katika mechi hiyo ambayo mashabiki wao waliamini wataendeleza ushindi.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Kondo alisema kabla ya kukutana na Yanga kuna vitu walikuwa makini kuwasoma wapinzani wao kwa kutazama uimara na upungufu wao ulipo.

Alisema waliwasoma vema na kubaini endapo watafanikiwa kudhibiti vema safu ya kiungo wao wa wapinzani hao watafanikiwa kupata ushindi jambo ambalo lilikwenda kama walivyopanga.

Alisema walifanikiwa kuhimili mchezo huo kwa dakika zote 90 kutokana na viungo wao kuwadhibiti ipasavyo wale wa Yanga huku mabeki nao wakitekeleza majukumu yao ipasavyo.

"Kikubwa tuliingia uwanjani tukihitaji pointi tatu ili tujiweke katika nafasi nzuri ya kuendelea kucheza Ligi Kuu msimu ujao, hivyo tuliwataka wachezaji watumie mapungufu ya Yanga kwa lengo la kupata alama tatu na hilo tulifanikiwa," alisema Kondo.

Alisema walifanikiwa kuimarisha upungufu wao hasa safu ya ushambuliaji na kufanikiwa kupata pointi tatu ambazo zimewaweka katika nafasi nzuri.

Kwa matokeo hayo, Yanga inabaki na pointi zake 50 huku ikiwa imecheza mechi 26, ikisalia kwenye nafasi ya tatu, lakini KMC ikichupa mpaka kwenye nafasi ya 16, kwa kufikisha pointi 30, ikicheza mechi 28, wakati huu ikiwa katika harakati ya kujiepusha kwenye janga la kushuka daraja.

Michezo

Jumamosi Machi 14, 2020

Nipashe




Arteta, Hudson-Odoi wapata coronavirus

UKURASA 30

MTANIKUBALI TU...



Mshambuliaji wa Manchester United, Mnigeria Odion Ighalo, akishangilia baada ya juzi kuifungia timu yake wakati ikishinda 5-0 ugenini Austria kwenye mechi ya Europa League hatua ya 16-bora dhidi ya LASK. Mabao mengine yalifungwa na Dan James, Juan Mata, Mason Greenwood na Andreas Pereira. **PICHA: MTANDAO**

# Msuva alia na corona Morocco

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI waziri wa afya wa Morocco jana akitangaza kuwa jumla ya watu saba nchini humo wamethibitika kuwa na virusi vya corona, mchezaji wa kimataifa wa Tanzania, Simon Msuva anayeichezea Klabu ya Difaa Hassani El Jadidi amewaomba Watanzania kumuombea kwa Mungu amnusuru na janga hilo.

Msuva aliyasema hayo jana, alipowasiliana na Nipashe kwa njia ya mtandao wakati huu akijiandaa kurejea nchini kuitumikia timu ya Taifa, Taifa Stars.

"Kiujumla ugonjwa wa Corona unatisha na kutuathiri kimchezo hasa ukizingatia huku kuna baadhi ya watu wamebainika kuwa nao, niombeeni nisikumbwe na janga hilo," alisema Msuva.

Alisema hatua ya kucheza bila mashabiki ni sawa kabisa kutokana na virusi hivyo kuambukizwa kwa njia ya hewa.

"Mashabiki wana raha yake uwanjani, lakini kwa sababu hiyo hakuna jinsi lazima wakatazwe ili ugonjwa usiwafikie wachezaji," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa ya waziri wa afya wa Morocco, ilieleza raia wa nchi hiyo ambao hivi karibuni walirejea nchini humo wakitokea Hispania walipimwa na kubainika kuwa na maambukizi chanya ya virusi vya corona ambavyo vilianzia mjini Wuhan, China Desemba mwaka jana. Corona, ambayo rasmi inajulikana kama COVID-19, vimeenea takriban nchi 123 huku kwa dunia nzima vifo vilivyotokana na ugonjwa huo vikielezwa kufikia 4,950, na watu zaidi ya 132,000 wakiwa na maambukizi kwa mujibu wa Shirika la Afya duniani (WHO) ambalo limeutangaza kama janga la dunia "global pandemic."

# YANGA WAMZINGUA EYMAEL, AITAJA SIMBA

## ●●● Awashukia wachezaji, Namungo yakoleza moto, yaionya huku ikieleza imewasoma...

**Na Saada Akida**

KIPIGO cha bao 1-0 kutoka kwa KMC FC katika Uwanja wa Uhuru juzi, wakati Yanga ikitoka kupata ushindi kama huo dhidi ya watani zao Simba, kimeonekana kumvuruga Kocha Mkuu wa miamba hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam, Mbelgiji Luc Eymael, imefahamika.

**Eymael amekuwa mbogo kwa wachezaji wake akiwataka kuwa makini wanapoingia uwanjani bila ya kudharau timu yoyote iwe kubwa ama ndogo.**

Na wakati kesho Yanga wakishuka katika Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi kukabiliana na Namungo FC, Eymael ameonekana kuvurugwa kabisa na matokeo ya mechi dhidi ya KMC, hivyo kutoa onyo kali kwa wachezaji wake akiwataka kamwe kutoishia kubweteka na ushindi walioupata dhidi ya Simba.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam kabla ya kikosi hicho kuelekea Lindi, Eymael alisema ataendelea kuwaonya wachezaji wake kwa kuwataka kuwa makini na timu zote bila kujali zilizoko juu yao ama chini ya msimamo ligi hiyo kwa kucheza mechi kama fainali.

Alisema hakuna timu ambayo ni rahisi kwa sasa, na kwamba wachezji wake walitumia nguvu nyingi katika mchezo dhidi ya Simba kwa kupata alama tatu, lakini wakashindwa kujituma kwa kucheza kwa kiwango bora katika mchezo dhidi ya KMC.

"Kuna faida gani kumfunga Simba halafu unapoteza baada ya ushindi huo, Simba ni nini, pointi tatu ndio muhimu, niliwaonya wachezaji wangu kabla ya kukutana na KMC kwamba si mchezo rahisi, pia naendelea kuwaonya kwamba mechi zilizopo mbele yetu ni ngumu kuliko ile ya Simba.

"Simba ni pointi tatu na michezo mingine iliyopo mbele yetu pia tunahitaji alama hizo hakuna kupumzika na kudharau, nimewataka wawe makini, naendelea kuwaonya wachezaji, huu mchezo hautakuwa rahisi, hivyo lazima wajitume kutafuta ushindi," alisema.

Alisema anahitaji kuhakikisha makosa yaliyofanyika katika mchezo wao uliopita hayajirudii katika mechi yao ya ugenini dhidi ya Namungo.

Naye Kocha wa Namungo, Thiery Hitimana, alisema amewaangalia wapinzani wao Yanga katika michezo miwili iliyopita, ilipocheza na Simba na kisha KMC na kuona tofauti, jambo ambalo litawalazimu kucheza nao kwa tahadhari kubwa.

Alisema katika michezo hiyo miwili, Yanga imecheza kwa viwango tofauti, hivyo hawatadanganyika na kiwango walichokionyesha dhidi ya KMC, na kwamba kwa upande wao wanajiandaa kutafuta matokeo mazuri katika uwanja wao wa nyumbani.

"Ni mechi ngumu kwetu na kwao pia, kwa upande wetu kupoteza kwa Yanga kumezidi kuifanya mechi yetu kuwa ngumu, lakini hilo halitusumbui kama kushambulia tutashambulia wote na kuzuia pia, kikubwa ni kuhakikisha tunatumia vema uwanja wetu wa nyumbani," alisema Thiery.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042